**Katibu** Mkuu CWT asimamishwa kazi tuhuma za utoro

UKURASA 3

**Anna** Tibaijuka akomalia hoja mgombea binafsi

UKURASA 3

**MIEZI 2 YA VITA:** UN yasema Gaza ni hatari kwa watoto

UKURASA 19


# Nipashe

Ijumaa Desemba 8, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581518

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




**BENCHIKHA ATEMA CHECHE, APATA DAWA 'KUIA' WYDAD**

UKURASA 23

# FARAJA KATESH

UKURASA 2

## Rais Samia aahidi... msafara wa Mbowe wakwamishwa kisha wamalizana.....



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga kuhusu athari za mafuriko yaliyotokea katika eneo la Jorodom Katesh, wilayani Hanang, alipotembelea eneo hilo, jana. **PICHA: IKULU**

## 'Balozi' mbaroni madai kuwakata vidole vijana watuhumiwa wizi nondo

UKURASA 7



## Prof. Shaba; bingwa aliyechunguza mwili wa Sokoine afariki

UKURASA 2

**MICHEZO** YANGA YASAKA POINTI MUHIMU CAF UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Jenista Mhagama (wa pili kushoto), akikabidhi misaada ya kibinadamu kwa wananchi waliopata maafa waliohifadhiwa katika Shule ya Sekondari Katesh, wilayani Hanang' mkoani Manyara juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Rais Samia apeleka faraja Katesh

**Na Waandishi Wetu**

"TUNATAMBUA na kujua dhiki, unyonge na ukiwa mnaoupitia, lakini hayo yote si yenu peke yenu ni dhiki yetu sote. Unyonge ni wetu sote na ukiwa ni wetu sote kama taifa."

Huyo ni Rais Samia Suluhu Hassan alipozungumza na waathirika wa mafuriko na maporomoko ya tope toka Mlima Hanang' wilaya Hanang', mkoani Manyara jana.

"Janga hili ni letu sote, na tumwombe Mwenyezi Mungu atuvushe salama katika mtihani huu mkubwa. Kama alivyosema Waziri Mkuu, serikali itaendelea kuchukua hatua kadhaa kuhakikisha eneo lililoathirika linarudi katika hali ya kawaida," alisema.

Baada ya kulazimika kukatisha ziara yake Dubai na kurejea nchini kutokana na maafa hayo, Rais Samia jana alitembelea maeneo yaliyoathirika, kuwapa pole majeruhi na kuhutubia wananchi.

Katika hotuba yake, Rais alisema janga hilo limeathiri kwa kiasi kikubwa mji mdogo wa Katesh ulioko makao makuu ya wilaya ya Hanang'.

Alibainisha kuwa janga hilo hadi kufikia jana mchana, lilikuwa limegharimu maisha ya watu 76, pia limeharibu makazi na mashamba ya wananchi.

"Lakini pia tumekuwa na majeruhi, nimetoka kuwatembelea hospitalini na tunashukuru kwamba wote wanaendelea vizuri. Kwa ujumla, janga hili pia limeharibu miundombinu ya barabara, umeme, maji na mambo mengine. Kwahiyo, ni janga kubwa ambalo limelikumba taifa letu," alisema.

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali itabaki katika eneo hilo na itakuwa bega kwa bega na wananchi mpaka itakapohakikisha hali imerudi kawaida.

"Lakini niseme mambo machache kwenu wananchi; kwa kawaida janga kama hili linapotokea, huwa kunatokea magonjwa ya mlipuko. Kwa sababu kilichosombwa huko, kilichochukuliwa, majumba yaliyochukuliwa huko yamechanganya vitu vingi, kwa kawaida hutokea magonjwa ya mlipuko.

"Niwaombe wananchi wote wa eneo hili kuchukua hadhari kubwa wakati mnapotumia maji na mambo mengine ili tusiwe na maradhi au magonjwa ya mlipuko," aliagiza.

Rais Samia alielekeza Wizara ya Maji kuhakikisha eneo hilo linakuwa na huduma ya majisafi na salama. Wizara ya Afya ihakikishe muda wote hakuna maradhi ya mlipuko yatakayotokea na yakijitokeza wawahi kwa haraka ili yasisambae.

"La pili ni kwamba majanga kama haya yanapotokea, huwa yanaleta mfadhaiko kwa wananchi.

"Hivyo basi, nimeitaka serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum kuleta wataalamu hapa ambao watazweza kuzungumza na tayari wapo, wazungumze na waathirika na wawarudishe katika hali ya kawaida.

"La tatu, nimewataka wananchi kufuatilia taarifa zinazotolewa na serikali kuu na serikali ya mkoa kuhusu hali ya hewa na kuchukua tahadhari ikiwamo kuondoka katika maeneo yote yaliyotokea maafa.

"Mkoa uwe makini kupata taarifa za hali ya hewa na kuzitoa kwa wananchi ili wananchi wachukue hatua stahiki tuepukane na haya yaliyotokea.

"Vyombo vya ulinzi ikiwezekana kuwe na ulinzi wa saa 24 katika maeneo yale yaliyozagaa tope ili kuwaepusha wananchi na hasa watoto kusogea katika maeneo hayo, kwa sababu nimezunguka na nimeona kwamba maeneo hayo si salama, kuna maeneo kuna mbonyeo na hatujui unakwenda mpaka wapi," aliagiza.

Mkuu wa Nchi pia alielekeza tahadhari iwekwe ili kukabili majanga kwa haraka, ikiwamo kuwa na akiba ya chakula ndani ya mkoa kabla serikali kuu haijaingia na kuongeza nguvu.

Vilevile, kutokana na maafa hayo, Rais Samia aliagiza serikali kuhakikisha kuanzia sasa inaongeza uwezo wake wa kukabiliana na maafa kwa vifaa na wataalamu katika kukabiliana na maafa ya aina hiyo.

Ni hoja iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Machi 2017 alipofanya ukaguzi kuhusu utayari wa nchi kukabiliana na majanga ya moto.

CAG pia alitoa pendekezo la kununuliwa vifaa na kuwa na rasilimali watu yenye mafunzo alipofanya Ukaguzi Maalum kuhusu Matukio ya Moto kwenye Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA), akibaini udhaifu kwa mamlaka (TANAPA) kukabiliana na majanga ya asili.

"Ninashukuru serikali katika maafa haya hatukupata msaada kutoka nje, tumeweza kufanya wenyewe na yote yanakwenda vizuri," alisema Rais Samia.

Awali Rais Samia alitembelea majeruhi waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya, akisisitiza kumrudia na kumshukuru Mungu licha ya mtihani huo waliopitia.

Aliwataka wauguzi wa hospitali hiyo kufanya kazi kwa bidii na kutoa huduma kwa wagonjwa hao kwa weledi.

Mmoja wa waathirika hao, Veronika Mefunya, alihoji hatua zinazochukuliwa na serikali ili wanapotoka kambini wasiendelee kuwa mzigo kwao, hasa katika kilimo na kusomesha watoto wao.

"Mimi pamoja na wenzangu tumepoteza vyeti vyetu vyote vya masomo. Je, serikali itatusaidiaje katika hilo?" alihoji Veronika aliyetaka kujua pia kama vijana wao watapatiwa ajira na serikali.

Katika majibu yake, Rais alisema serikali haitowaacha, akiagiza wakuu wa wilaya kuwasaidia wale waliopoteza vyeti wapate vingine. Alielekeza waende katika taasisi za elimu husika na kutoa taarifa zao sahihi.

"Kila aliyepoteza vyeti, ninaomba wakuu wa wilaya mshughulikie. Kuhusu watoto kwenda shule serikali itaangalia na kuwapatia vifaa muhimu vinavyohitajika kwa kuwa elimu inatolewa bure," alisema Rais Samia huku akisisitiza uhaba wa ajira kwa vijana ni changamoto ya kitaifa. Suluhisho ni kujiajiri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Jenista Mhagama, alisema kwa mujibu wa uchunguzi wa kijiolojia uliofanyika, wamearifiwa na Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kwamba katika tukio hilo hakukuwa na tetemeko la ardhi wala mlipuko wa volcano katika Mlima Hanang'

"Miamba hiyo ilinyonya maji ya mvua na kuporomoka, na hivyo kutengeneza tope kubwa, na kipande hicho kilichomeguka kilinyonya maji na kusababisha mgandamizo na sehemu ya mlima, ikashindwa kuhimili mgandamizo huo na hivyo kutengeneza tope lililoanza kuporomoka kwa kasi na kutengeneza njia kufuata mkondo wa Mto Jorodom," alisema.

Waziri huyo alimweleza Rais Samia kwamba majanga hayo yamesababisha vifo vya watu 76, majeruhi 117 na kaya 1,150 zenye wakazi wapatao 5,600 zimeathirika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza kabla ya kumkaribisha Rais Samia, alisema wataendelea kutoa huduma kwa waathirika wote na kuhakikisha wanarejesha huduma, uendeshaji wa shughuli za kiuchumi na shughuli za kijamii.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, alisema ziara ya Rais ni faraja kwa Katesh na Kata zilizopata changamoto ya maporomoko ya tope, mawe, magogo, miti na maji.

**MSAFARA CHADEMA**

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, Mbunge wa zamani wa Arusha, Godbless Lema, Katibu wa Kanda wa chama hicho, Amani Golugwa na viongozi wa Jimbo la Mbulu, jana walidai kuzuiwa kwa muda kuingia Katesh na Jeshi la Polisi, lakini baadaye wakaruhusiwa kutembelea majeruhi katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara na Hospitali ya Wilaya ya Hanang' (Tumaini).

Lema alidai baadhi ya magari yao yalishikiliwa na baadaye walikwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa, walikokumbana na vikwazo, lakini mmoja wa viongozi wakubwa serikalini aliwapigia simu akaomba radhi kutokana na kilichotokea. Wakarejea kutoa pole kwa waathirika.

***Imeandaliwa na Jaliwasson Jasson (MANYARA), Godfrey Mushi (ARUSHA) na Jenifer Gilla (DAR).**

## Prof. Shaba; aliyechunguza mwili wa Sokoine afariki dunia

**Na Christina Mwakangale**

DAKTARI Bingwa wa Tiba ya Binadamu mbobezi katika uchunguzi wa miili ya binadamu, Prof. James Shaba, amefariki dunia.

Taarifa kuhusu kifo cha mtalaamu huyo bingwa zinasema Prof. Shaba alifariki Jumanne wiki hii nchini Marekani na mwili wake unatarajiwa kurejeshwa nchini kwa maziko.

Prof. Shaba aliyejizolea umaarufu katika stadi ya kuutambua mwili wa binadamu na sababu za kifo, aliitumikia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa miaka mingi kabla ya kustaafu. Moja ya rekodi zake zinazomtambulisha ni uchunguzi wa kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Edward Sokoine, April 12, 1984.

Mwanafamilia Maria Shaba, akizungumza na Nipashe jana, alisema maandilizi yanaendelea ya kuuleta mwili nchini, kutoka Chicago, Marekani, alikokuwa akiishi.

"Taarifa kuhusu mazishi yanavyoendelea, kuwasili kwa mwili na maziko, tusubiri kutoka kwa walioko Chicago. Amefia huko Marekani, taarifa zikipatikana zaidi tutaziwasilisha," alisema Maria.

kwa mujibu wa taarifa za awali, Prof. Shaba alikuwa akiishi Marekani, ambako kuna watoto wake.

Awali, mtoto wa marehemu, Anale Shaba, alisema: "Mzee wetu ametutoka jioni siku ya Jumanne tarehe 5 Decemba 2023, muda wa saa 2:30 usiku saa za Marekani (Central Eastern Time) Chicago. Habari zaidi za maandalizi ya mazishi zitatumwa baadaye.

"Mzee alikuwa akiuguzwa na watoto wake Stella na Anale Shaba, kwa muda mrefu. Mungu aipumzishe roho ya mzee wetu mahali pema peponi. Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe," ilimaliza taarifa hiyo.

# Prof. Tibaijuka akomalia mgombea binafsi

**Na Zanura Mollel**

WAZIRI wa zamani wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Prof. Anna Tibaijuka, amesema uwapo wa mgombea binafsi katika nafasi mbalimbali za kisiasa, kutapunguza ukatili wa kijinsia wanaoukumbana nao wanawake kipindi cha uchaguzi ikiwamo rushwa ya ngono.

Prof. Tibaijuka alisema hayo jana kwenye mafunzo yaliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TNGP) mkoani Dar es Salaam, yaliyolenga kupinga ukatili wa kijinsia, upatikanaji wa chombo kimoja kitakachowakutanisha wanawake wote na kupanga mikakati yao na kuwa na sauti ya pamoja.

"Ukiombwa rushwa ya ngono ukikataa nani atakulazimisha? Hii kauli ya kuwa wanawake hawapendeni ni propaganda tu za kutugawa," alisema.

Prof. Tibaijuka alisema kupigania haki ya wanawake ni jambo endelevu na kwamba wanawake wameonekana kufanyiwa dhuluma katika nafasi mbalimbali za uongozi kwa kufichiwa fomu za kuwania nafasi za uongozi.

"Takwimu za wanawake waliochukua fomu kuwania nafasi za uongozi kipindi cha uchaguzi hazionekani na wala huwezi kupata sababu kwa nini zinafichwa? Wanaficha kwa sababu wanafahamu mwanamke akipewa nafasi atashinda," alisema.

"Lakini pia mfumo wa vyama vingi ndio uliotufikisha kwenye matatizo haya ya wanawake kuminywa kwenye nafasi za kisiasa kutokana na mfumo dume ulioukwa pamoja na uwoga uliopo ndani ya vyama hivyo.

"Rais Dk. Samia akimsaidia mwanamke kwa kupatikana kwa katiba mpya atakuwa amemsaidia mwanamke kupata mgombe binafsi," alisisitiza.

Akiwasilisha taarifa ya hali ya ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi wa kisiasa Tanzania, Prof Alexander Makulilo alisema kuanzia mwaka 1995 hadi 2023 uchaguzi wa wanawake ubunge majimboni na viti maalumu waliopaya nafasi ni 106.

"Mwaka 1995 walikuwa wanane, 2000 walikuwa 12, 2005 walikuwa 17, mwaka 2010 walikuwa 21, 2015 walifikia 25 na 2020 ni 26," alisema.

Pia alisema uchaguzi wa mwaka 2020 vyama vilivyoshiriki kwenye uchaguzi wa urais vilikuwa 15 na wanawake wawili walijitokeza kugombea nafasi hiyo huku wagombea wenza wakiwa watano.

Katika nafasi ya ubunge, walijitokeza wagombea 1,257 wanawake wakiwa 239 na wanaume 964 katika majimbo 264 huku waliojitokeza kwenye udiwani walikuwa 9,231 wakiwamo wanawake 669

Prof. Mkulilo aliainisha baadhi ya sababu zilizochangia wanawake kutojitokeza kugombea ni pamoja na upungufu katika mfumo wa sheria, ukatili wa kijinsia (rushwa ya ngono na udhalilishwaji), msukumo mdogo kutoka kwa uongozi wa juu, hali ya uchumi, kukosekana kwa taarifa, kufananisha siasa na mfumo dume.

"Lakini pia mfumo ni kikwazo kwa sabau kwa Tanzania mtu hawezi kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa kama hayuko kwenye chama cha siasa," alisema.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Gairo,mkoani Morogoro, Rachel Nyangasi, alisema ukatili bado unaendelea ndani ya jamii na wazazi wameonekana kuwakatili watoto wa kike kwa kuwaamuru kutofanya vizuri kwenye mitihani ya mwisho ya kuhitimu darasa la saba.

"Hali hii iko kwenye halmashauri yangu lakini tumeweka mpango wa kuzungumza na watoto hawa pamoja na kuwapa elimu. Kampeni yetu inaitwa 'Kutokomeza Zero kwa Wanafunzi Wanawake Darasani", alisema.

Mwakilishi Baraza la Vyama vya Siasa, Abdul Mluya, alisema katika kupinga ukatili kwa watoto ili wapate elimu ni wakati wa jamii kujitathmini na kukataa kutoa ajira kwa watoto.

Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, Lilian Lihundi, alisema takwimu zilitolewa na Umoja wa Mataifa mwaka 2016 zilionyesha kupotea kwa Dola za marekani trilioni 1.5 ambazo hutumika kutokomeza ukatili wa kijinsia.

"Benki ya Dunia (WB) mwaka 2018 ilisema asilimia 3.7 za fedha Afrika hugharimu kila nchi kwe-

# Katibu mkuu CWT asimamishwa kazi na mwajiri madai ya utoro

**Na Romana Mallya**

TUME ya Utumishi ya Walimu (TSC) imemsimamisha kazi Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mwalimu Maganga Japhet, ambaye pia ni mwalimu wa Shule ya Msingi Tandika, Temeke mkoani Dar es Salaam.

Taarifa kwa umma iliyotolewa iliyotolewa Jumanne na Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Manispaa ya Temeke, Francis Mselemo, ilisema Japhet amesimamishwa kazi kwa tuhuma za utoro kazini na kukaidi maelekezo halali ya viongozi wake.

Januari 25, mwaka huu, Japhet alikuwa miongoni mwa wateule wa Rais katika nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa mkoani Kagera lakini hakwenda kuapa ili kuanza utekelezaji wa majukumu hayo.

"Mkurugenzi wa Halmashauri wa Manispaa ya Temeke, Elihuruma Mabelya, anapenda kuufahamisha umma kuwa, TSC ambayo ndiyo mamlaka ya nidhamu ya walimu, imemsimamisha kazi mwalimu Maganga Moses Japhet tangu Desemba 5, mwaka huu," ilisema taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Mwalimu Japhet amesimamishwa kazi kutokana na tuhuma za utoro kazini na kukaidi au kukataa maelekezo halali ya viongozi wake.

Oktoba 16, mwaka huu, Mabelya aliliambia Nipashe kuwa, Japhet ni mtumishi wa Manispaa ya Temeke na alitakiwa kuripoti kazini Oktoba Mosi, mwaka huu, kama alivyotakiwa katika tangazo la wito lakini hadi wakati huo alikuwa hajaripoti.

"Hatujawahi kumwona tunaendelea na utaratibu wetu wa ndani.

Sisi tunajua ni mfanyakazi wa Temeke na kinachofanyika ni kuchukua hatua za kinidhamu. Mchakato wa kufungua shauri la kinidhamu unaendelea.

"Yule ni mtumishi wa serikali hapaswi kuigomea serikali.

Sisi tunachojua yeye ni mtumishi wetu kule aliko kibali kimeisha si tena sehemu yake ya kazi," alisema.

Oktoba 3, 2023, mkurugenzi huyo alisema Japhet asiporejea baada ya siku saba tangu alipotakiwa kufanya hivyo, atafunguliwa shauri la nidhamu.

Wakati uongozi wa manispaa ukisema hivyo, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema bado hawajapokea barua ya kumtaka Japhet kurejea katika kituo chake cha kazi na anaendelea na majukumu yake ya Katibu Mkuu wa CWT.

"Kwanza sijajua ile nyaraka iliyoonekana ilikuwa ni barua au tangazo kwa sababu ili hatua zozote zichukuliwe ni lazima kuwe na mchakato halali ili kufanyia kazi.

"Suala la kibali ni mwajiri na mwajiriwa wake, na atamjulisha kwamba nakubali uendelee au sikubali sasa mwajiriwa hajapata na wala sisi hatuna nakala. Kwa hiyo hatuwezi kuchukua hatua zozote na sisi hatuna chochote tunachojua zaidi ya kujua kwamba ni Katibu Mkuu ataendelea kuwapo na kazi zinaendelea," alisema.

Septemba 25, 2023 siku ya kikao cha Baraza la Dharura la CWT jijini Dodoma, Nipashe ilimtafuta Japhet kuhusu suala hilo na kujibu kuwa bado hajapewa barua ya kukataliwa kwa ombi lake la kuendelea kuazimwa na chama hicho.

Septemba 23, 2023, Mabelya alitoa tangazo akimtaka Japhet kurejea kwa mwajiri wake ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu, baada ya serikali kutokubali maombi yake ya kuendelea kuazimwa na CWT.

Katika tangazo hilo, inaonyesha Japhet aliomba na kibali cha kuazimwa na CWT Agosti, 2017 kilichomalizika Septemba 30, 2020.

Aidha, Japhet aliomba nyongeza ya kibali cha kuanzia Juni Mosi, 2020 na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Utumishi alimpa nyongeza Agosti 10, mwaka 2020, kinachoishia Septemba 30, mwaka huu.

Tangazo hilo linasema Maganga ambaye cheo chake ni mwalimu mwandamizi, aliomba tena kibali cha kuazimwa kwa mara ya tatu, lakini Katibu Mkuu Utumishi hajaridhia maombi hayo.

"Hivyo basi Mwalimu Japhet Maganga anapaswa kurejea kwenye kituo chake cha kazi mara moja Oktoba Mosi, 2023," lilisema tangazo hilo.

Wengine walioteuliwa na Rais Januari 25, mwaka huu, walikuwa Makamu wa Rais wa CWT, Dinna Mathaman, na Rais wa CWT, Leah Ulaya, lakini ni Dinna pekee alikwenda kuapa kushika nafasi ya ukuu wa wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Leah aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita.




MWENYEKITI MTENDAJI, MENEJIMENTI NA WAFANYAKAZI WOTE WA KAMPUNI ZA IPP TUNAUNGANA NA WATANZANIA WENZETU KUTOA POLE KWA WANANCHI WA HANANG MKOANI MANYARA KUTOKANA NA MAFURIKO YALIYOSABABISHA VIFO, MAJERUHI NA UHARIBIFU MKUBWA WA MALI. MWENYEZI MUNGU AWAPE MAJERUHI UPONYAJI WA HARAKA NA KUWAPA PUMZIKO LA MILELE MAREHEMU WOTE, AMINA

IPP

# Prof. Tibaijuka: Vita kupinga ukatili jinsia isimweke kando mtoto wa kiume

**Na Elizabeth Zaya**

MBUNGE wa zamani wa Muleba Kusini, Prof. Anna Tibaijuka, amesema kuna haja kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watoto wa kiume kama ilivyo sasa kwa watoto wa kike.

Prof. Tibaijuka alitoa kauli hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia lililoratibiwa na Mtandao wa Kupinga Ukatili wa Kijinsia (MKUKI) kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF).

Mwanasiasa huyo aliyewahi kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema katika mapambano hayo ya ukatili wa kijinsia, ni vyema mtoto wa kiume naye akaangaliwa kwa kuwa naye yuko kwenye hatari kubwa.

"Na kwa sasa kuna presha kubwa ya malezi kwa mtoto huyu wa kiume, ninaomba tuliangalie nalo hilo na katika kipindi hiki cha siku 16 kutoa elimu pamoja na mapambano dhidi ya ukatili, tujikite huko pia," alitoa angalizo.

Kuhusu ukatili wa kijinsia kwa watoto wa kike na wanawake, Prof. Tibaijuka alisema chanzo kikubwa kiko nyumbani pamoja na jamii kuendelea kukumbatia mila, desturi na utamaduni uliopitwa na wakati.

"Kama ambavyo mnasema namna wanawake wanavyopitia ukatili kwenye siasa, lakini niwakumbushe kwamba ukatili huohuo pia unaanzia nyumbani na si kwenye siasa wala kazini pekee.

"Ukatili dhidi ya mwanamke unaanzia nyumbani kwenye familia. Kwahiyo, tunapoangalia ukatili wa mwanamke tufahamu kuwa pia kuna utamaduni unaofifisha uwezo wa mwanamke, makuzi na malezi ambayo yanamfanya ajione yeye hafai," alionya.

Prof. Tibaijuka alisema vita vya ukatili wa kijinsia ni sawa na kupigania uhuru, hivyo nguvu ya pamoja inahitajika katika hilo.

"Kwahiyo, katika kipindi hiki cha kupinga ukatili wa kijinsia, tuzungumze, tutumie hata wanawake wanasheria, majaji na wengine waliopata nafasi kuelezea uwezo wa mwanamke huyu.

"Tusiangalie tu ukatili wa mwanamke kwenye siasa au sehemu za kazi, tuangalie mwanamke pale alipo," alisema Prof.Tibaijuka.



Ofisa Mtendaji Mkuu mpya wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Adam Mihayo (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mipango ya Benki hiyo, Muondakweli Kaniki (kulia), aliporipoti rasmi kazini, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii baada ya kuteuliwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hiyo. Wa pili kulia ni Mkurugenzi Rasilimali Watu wa Benki hiyo, Diana Myonga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CTI yaonesha matumaini ujenzi wa reli ya kisasa

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini (CTI) limeeleza kufurahishwa na kasi ya ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), likisema kuwa itasaidia kuharakisha ukuaji wa uchumi na biashara.

Jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa shirikisho hilo, Leodegar Tenga, alieleza kufurahishwa na mradi huo baada ya wanachama wa shirikisho hilo kutembelea reli hiyo kuanzia Dar es Salaam hadi Kwala, Mkoa wa Pwani.

Tenga alisema CTI iliamua kupanga ziara hiyo baada ya wanachama wake wengi kuomba kwenda kutembelea reli hiyo ili kuona hatua ya ujenzi iliyofikiwa.

"Tumefurahishwa sana na kinachoendelea ni dhahiri sasa tumefikia hatua za mwishomwisho na hivi karibuni tutaanza kuona matunda ya mradi huu mkubwa na kwa kweli TRC (Shirika la Reli Tanzania) wanafanya kazi nzuri sana," alisema.

Tenga alitaja moja ya faida za mradi huo kuwa ni kusafirisha bidhaa na mizigo mingi kwa haraka kutoka kwenye viwanda na kupeleka kwa wateja kwenye mikoa mbalimbali na nje ya nchi.

Alisema wenye viwanda wamekuwa wanasubiri kwa hamu kukamilika mradi huo kwa kuwa utawasaidia kusambaza bidhaa zao ndani ya muda mfupi tofauti na sasa ambapo mizigo inakaa muda mrefu barabarani.

"Hii SGR itasaidia sana ukuaji wa uchumi kwa kasi kwa sababu kama viwanda vitasafirisha bidhaa zake kwa wingi na kwa muda mfupi, ina maana vitafanya biashara sana na kuingiza kodi nyingi kwa serikali na idadi ya ajira pia itaongezeka. Kwa hiyo, ninawapongeza TRC kwa kazi nzuri.

"Ingawa sisi tupo hapahapa Dar es Salaam, lakini ni mara yetu ya kwanza kuja kuona mradi huu na kwa kweli tumeshangazwa na hatua kubwa waliyofikia na tunatarajia kama watakwenda na kasi hii, ni matumaini yetu kuanzia mwakani tutaanza kutumia reli ya SGR," alisema.

Mkurugenzi wa Tanzania Meat Product (2002), Evarist Maembe, alisema reli hiyo itakuwa msaada mkubwa kwenye uchumi wa nchi na alipongeza TRC kwa kazi kubwa ya kutekeleza mradi huo usiku na mchana.

Alisema ili wenye viwanda wafanye biashara kwa uhakika, wanahitaji usafiri wa haraka na wa uhakika, hivyo kukamilika kwa reli hiyo kutaleta ahueni kubwa kwa wenye viwanda na wafanyabiashara.

"Usafiri wa maroli hauwezi kukusaidia kusafirisha mzigo mkubwa na kwa wakati, Reli ndiyo kila kitu, ni kama ilivyo kwa umeme, bila umeme huwezi kufanya kitu kwenye uzalishaji," alisema Maembe

Stela Nyaki kutoka kampuni ya KAMAL alisema reli ya kisasa ni mradi ambao umekuwa kiu ya watu wengi ambao wangependa kusafirisha bidhaa zao kwa wingi na kufika kunakostahili kwa wakati. Alisema kukamilika kwa mradi huo kutawezesha baadhi ya watu kuishi mkoani Morogoro na kufanya kazi jijini Dar es Salaam kwa kuwa treni itakuwa inachukua muda wa saa moja kwenda na kurudi kwenye mikoa hiyo miwili.

"Kukamilika kwa reli hii kutakuwa fursa kubwa sana kwetu wafanyabiashara na wenye viwanda na kwa maelezo ambayo tumeyapata mradi utakamilika hivi karibuni na watu wataanza kufaidi matunda ya reli hii," alisema Stela.

# Anayedaiwa kutoroka polisi akiwa na pingu, asomewa shtaka jipya

**Na Samson Chacha,** TARIME

MTUHUMIWA wa wizi wa mchanga wenye madini ya dhahabu yenye thamani ya Sh. milioni 77.5 toka Mgodi wa Barrick North Mara, mkoani Mara, Raphael Zakaria, maarufu Man K, amekamatwa tena na kufikishwa mahakamani na kusomewa kosa la kutoroka akiwa chini ya ulinzi halali.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kutoroka akiwa chini ya ulinzi wa polisi akiwa na pingu wakati wakitoka mahakamani akiwa na wenzake.

Akimsomea shtaka hilo katika kesi ya jinai juzi mbele ya Hakimu mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Stanel Mwakihaba, Mwendesha Mashitaka wa Serikali, Davis Katesigwa, alidai:

"Mtuhumiwa Raphael Matiko Zakaria ambaye anatuhumiwa katika kesi nyingine ya awali ya wizi katika Mgodi wa Barrick North Mara inayoshirikiana na kampuni ya Twiga Minerals, akiwa na wenzake saba, waliiba mchanga wenye dhahabu gramu 574.87 na dhahabu yenye uzito wa gramu 17.934 yenye thamani ya Sh. milioni 77.5.

"Mtuhumiwa na wenzake walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya Tarime mnamo Novemba 13, 2023 na kesi yao kupangiwa tarehe nyingine.

"Wakati wakirejea gerezani, mtuhumiwa Raphael Matiko alitoroka askari polisi akiwa chini ya ulinzi halali na pingu na kutokomea kusikojulikana.

"Juhudi za kumtafuta zilianza mara moja na kufanikiwa kumkamata na kufikishwa mhakamani hapa," alidai.

Mwendesha mashtaka huyo alidai kuwa mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka ya kutoroka chini ya ulinzi halali chini ya kifungu Na. 116 na 35 vya Sheria ya Kanuni za Adhabu, marejeo ya mwaka 2022 na anatakiwa kusomewa maelezo ya awali mbali na kudai kuwa hajisikii vyema kiafya. Hakimu wa mahakama hiyo, Mwakihaba, alisema, "kwa kuwa mshtakiwa anadai hali yake si nzuri hajisikii vyema, ninapanga tarehe 18 Desemba, 2023 aje asomewa maelezo hayo ya awali katika kesi yake hiyo na ataendelea kuwa mahabusu," Hakimu Mwakihaba alisema.

TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inapenda kuutangazia umma kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa kifungu cha 4(2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 amefanya mabadiliko katika orodha ya viongozi wanaotambulika kwa mujibu wa Sheria. Orodha mpya ya viongozi kama ilivyotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 857 la tarehe 24.12.2023 ni hii iliyo chapishwa katika gazeti hili, vile vile inapatikana katika tovuti ya Taasisi ambayo ni www.maadili.go.tz. Watumishi wa umma kwenye Wizara, Idara za Serikali, Taasisi za Umma, Mamlaka za Serikali, Wakala za Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanaombwa kupitia ili kuona kama nyadhifa walizonazo kwa sasa zinatambulika kama Viongozi wa Umma.

Viongozi wote wa Umma wanapaswa kuzingatia misingi inayoainishwa chini ya Sheria ikiwemo kutoa tamko la Rasilimali na Madeni.

**Imetolewa na:** **KAMISHNA WA MAADILI**
**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**
**7 Desemba, 2023**

*Notisi ya Kubadili Orodha ya Viongozi wa Umma Katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 857 la tarehe 24/11/2023

SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA,
(SURA YA 398)

### NOTISI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 4)*

NOTISI YA KUBADILI ORODHA YA VIONGOZI WA UMMA KATIKA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA YA MWAKA 2023

Jina
Sura ya 398

1. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Kubadili Orodha ya Viongozi wa Umma katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 2023 na itasomwa pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo hapa itarejewa kama "Sheria".

Kubadili orodha

2. Orodha ya nyadhifa za umma iliyoainishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria, katika tafsiri ya neno "kiongozi wa umma", inabadilishwa kwa kufutwa na badala yake kuwekwa orodha ifuatayo:

"

(i) Rais wa Jamhuri ya Muungano;
(ii) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;
(iii) Rais wa Zanzibar;
(iv) Waziri Mkuu;
(v) Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar;
(vi) Spika, Naibu Spika na Mbunge;
(vii) Jaji Mkuu, Jaji wa Rufani, Jaji wa Mahakama Kuu na Hakimu;
(viii) Waziri, Naibu Waziri, Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya;
(ix) Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
(x) Balozi Mwakilishi wa Tanzania nchi za Nje;
(xi) Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Tawala wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa Msaidizi na Katibu Tawala wa Wilaya;
(xii) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Nje;
(xiii) Katibu wa Bunge;
(xiv) Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi;
(xv) Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi;
(xvi) Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa;
(xvii) Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza;
(xviii) Kamishna Jenerali wa Uhamiaji;
(xix) Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji;
(xx) Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za kulevya;
(xxi) Mkurugenzi Mkuu wa Usalama wa Taifa;
(xxii) Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; Mkuu wa TAKUKURU Mkoa na Mkuu wa TAKUKURU Wilaya;
(xxiii) Afisa katika Jeshi la Ulinzi kuanzia cheo cha Kanali;
(xxiv) Afisa katika Jeshi la Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zimamoto na Uokoaji kuanzia cheo cha Kamishna Msaidizi;
(xxv) Kamanda wa Polisi Mkoa, Mkuu wa Upelelezi Mkoa, Mkuu wa Usalama Barabarani Mkoa, Mkuu wa Polisi Wilaya, Mkuu wa Upelelezi Wilaya na Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya;
(xxvi) Mkuu wa Magereza Mkoa na Mkuu wa Gereza;
(xxvii) Gavana na Naibu Gavana;

*Notisi ya Kubadili Orodha ya Viongozi wa Umma Katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

*Tangazo La Serikali Na. 857 (Linaendelea))*

(xxviii) Mtendaji Mkuu na Naibu Mtendaji Mkuu katika Taasisi, Idara, Mamlaka, Wakala wa Serikali, Shirika na Kampuni ya Umma;
(xxix) Mwakilishi wa Serikali katika Shirika au Kampuni ambayo Serikali ina Maslahi;
(xxx) Meya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Diwani;
(xxxi) Mkurugenzi, Naibu Mkurugenzi, Mkurugenzi Msaidizi, Katibu, Naibu Katibu, Katibu Msaidizi na Meneja katika Wizara, Taasisi ya Umma, Idara ya Serikali, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(xxxii) Mkuu wa Idara au Kitengo katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(xxxiii) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mjumbe au Kamishna katika Tume;
(xxxiv) Msajili, Mrajisi, Naibu Msajili, Naibu Mrajisi, Msajili Msaidizi, Mrajisi Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Shirika la Umma, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(xxxv) Kamishna na Kamishna Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali na Wakala wa Serikali;
(xxxvi) Katibu Binafsi na Naibu Katibu au Katibu Msaidizi Binafsi wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;
(xxxvii) Mshauri wa Rais;
(xxxviii) Msaidizi wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;
(xxxix) Mwandishi wa Habari, Mwandishi wa Habari Msaidizi na Mpiga Picha wa Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu;
(xl) Mratibu, Mratibu Msaidizi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka na Wakala wa Serikali;
(xli) Mratibu wa Mradi katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa;
(xlii) Mnikulu na Naibu Mnikulu;
(xliii) Karani na Naibu Karani wa Baraza la Mawaziri;
(xliv) Msaidizi wa Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza la Mawaziri;
(xlv) Mganga Mkuu na Mfamasia Mkuu wa Serikali, Mganga Mkuu wa Mkoa, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kanda, Mkoa na Wilaya;
(xlvi) Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali Msaidizi na Mkuu wa Hazina Ndogo na Mhakikimali wa Mkoa na Wilaya.
(xlvii) Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali Msaidizi;
(xlviii) Msajili Mkuu, Msajili na Naibu Msajili wa Mahakama;
(xlix) Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Mtendaji wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu;
(l) Mwandishi Mkuu wa Sheria;
(li) Msajili wa Hazina;
(lii) Mhasibu Mkuu na Mkaguzi wa Ndani Mkuu katika Wizara, Idara ya Serikali, Taasisi ya Umma, Shirika la Umma, Mamlaka ya Serikali, Wakala wa Serikali, Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

*Notisi ya Kubadili Orodha ya Viongozi wa Umma Katika Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma*

*Tangazo La Serikali Na. 857 (Linaendelea))*

(liii) Makamu Mkuu wa Chuo, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Mkuu wa Kampasi, Mkuu wa Ndaki, Mkuu wa Kitivo na Mkuu wa Shule katika Chuo Kikuu cha Umma;
(liv) Mkuu wa Chuo, Naibu Mkuu wa Chuo, Mkuu wa Kampasi, Mkuu wa Ndaki na Mkuu wa Kitivo katika Taasisi ya Elimu;
(lv) Mthamini Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi na Nyumba wa Wilaya;
(lvi) Afisa Usalama Mkoa na Wilaya;
(lvii) Mkurugenzi wa Mashtaka, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Mkuu wa Mashtaka Mkoa na Mwendesha Mashtaka Wilaya;
(lviii) Wakili Mkuu wa Serikali na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali;
(lix) Kabidhi Wasii Mkuu na Naibu Kabidhi Wasii Mkuu;
(lx) Msuluhishi na Muamuzi katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi;
(lxi) Afisa Madini Mkazi; na
(lxii) Mwenyekiti na Mjumbe wa Bodi katika Bodi ya Wakurugenzi na Bodi ya Wadhamini katika Taasisi ya Umma.".

Kufuta TS. Na. 209 la 2005 260 la 2013

3. Notisi ya Mabadiliko ya Orodha ya Viongozi wa Umma ya Mwaka 2005 na Notisi ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Nyongeza ya Orodha ya Viongozi wa Umma) Taarifa, 2013 zinafutwa.

Dodoma,
28 Agosti, 2023

SAMIA SULUHU HASSAN
*Rais*

217746802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hadhari, hatua zichukuliwe dhidi ya mvua zinazonyesha

**MADHARA** yanayotokana na mvua inayoendelea kunyesha yanaongezeka siku hadi siku huku baadhi ya wananchi katika maeneo mbalimbali wakipoteza maisha na wengine kukosa makazi.

Maafa zaidi yametokea katika mkoa wa Manyara wilayani Hanang baada ya maporomoko ya tope kutoka Mlima Hanang kuathiri mji wa Katesh. Kutokana na madhara hayo, hadi juzi watu 69 walipoteza maisha huku ikibainishwa kuwa kuna kijiji ambacho kimeathirika zaidi kwa nyumba nyingi na miundombinu ya taasisi kuharibiwa vibaya.

Hali kama hiyo pia imeripotiwa katika wilaya ya Shinyanga mikoani Shinyanga na Kilosa, Morogoro ambako iliripotiwa juzi kwamba watu wawili walifariki dunia kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zilizonyesha katika maeneo hayo. Sambamba na vifo hivyo, taarifa zimeeleza kuwa nyumba 51 zimeanguka kutokana na mvua ya mawe iliyonyesha.

Pamoja na kuripotiwa mvua katika maeneo mbalimbali kwa siku za karibuni, siku chache zilizopita pia ilibainishwa kuwa mvua kama hizo zilinyesha katika mikoa ya Tanga, Morogoro na Arusha na kusababisha vifo vya watu kadhaa na mali kuharibiwa. Maafa makubwa zaidi katika mvua hizo yalitokea mkoani Arusha baada ya watu kadhaa kufariki dunia na mali mbalimbali kuharibiwa pamoja na wananchi kukosa makazi.

Maafa yaliyotokea Hanang kutokana na tope la mafuriko ni makubwa zaidi kuripotiwa nchi hii. Maafa hayo yamesababisha serikali kuelekeza nguvu katika eneo hilo kwa kupeleka vikosi vya uokozi na misaada mbalimbali ya kibinadamu. Pia wadau mbalimbali wakiwamo vyama vya siasa, Bunge na taasisi za dini wamepeleka misaada yakiwamo magodoro, sabuni, vyakula na dawa kwa ajili ya waathirika wa mafuriko hayo.

Maafa yaliyoripotiwa katika wilaya ya Hanang ni makubwa kutokea kwa miaka mingi katika historia ya Tanzania na yametoa somo kubwa juu ya kujikinga na maafa pindi mamlaka husika zinapotangaza. ivi Hivi karibuni, mathalan, Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitangaza tishio la kuwapo kwa mvua kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi kuanzia Oktoba, mwaka huu.

Matokeo ya utabiri huo yameonyesha ukweli wa jambo lenyewe kwamba kutakuwa na mvua kubwa katika maeneo mbalimbali ambayo itasababisha hasara kubwa kwa miundombinu, vifo vya binadamu na wanyama hata baadhi ya maeneo kukosa makazi. Matokeo ya utabiti huo yamesadifu na uhalisia wa sasa baada ya maeneo kadhaa nchini kukumbwa na mvua ambazo zimesababisha madhara mbalimbali.

Kama TMA ilivyosema kwamba tahadhari zinapaswa kuchukuliwa, ni wakati mwafaka sasa kwa vikosi vya uokoaji kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, kamati za maafa katika ngazi mbalimbali na wananchi kwa ujumla kutekeleza hilo.

Yako maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa yakikumbwa na mafuriko au kupata madhara pindi mvua zinaponyesha kwa sababu tu ya miumdombinu ya kusafirisha maji ya mvua kujaa uchafu, hivyo kusababisha maji kufurika kwa sababu ya kukosa njia.

Miongoni mwa maeneo hayo yako Dar es Salaam, hivyo uongozi wa mkoa, wilaya hadi mitaa unapaswa kuliangalia jambo hilo kwa jicho la kipekee ili madhara makubwa yasiwapate wananchi.

Aidha, katika barabara kuu zinazounganisha mikoa mbalimbali, maji ya mvua yamekuwa yakijaa hadi kwenye miundombinu hiyo pamoja na kubomoa madaraja. Matokeo yake husababisha usafiri kuwa wa shida na wakati mwingine watu kupoteza maisha.

Kuna msemo kwamba tahadhari kabla ya hatari. Yaliyotokea Katesh yapaswa kuwa funzo kwa Watanzania na kuchukua hatua za kujihami kabla ya kutokea madhara kama hayo. Wale wanaoishi mabondeni kama Dar es Salaam, wanapaswa kuchukua hatua kwa kuwa inatabiriwa kuwa kuna uwezekano wa mvua kubwa kunyesha na kusababisha maafa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Msimu wa kilimo ndio huo, wenye mashamba jiandaeni na mbegu bora

Na Halfani Chusi

**MSIMU** wa kilimo umefika sasa, wakulima tuingie shamba, lakini angalizo langu, ili uweze kupata kipato kikubwa kulingana na eneo, lazima utumie mbegu kuzalisha nafaka na sio nafaka kuigeuza mbegu.

Nilihuduhuria semina iliyowakutanisha wataalamu wa kilimo. Moja ya hoja iliyopamba moto kwenye ukumbi huo, ilikuwa wakulima wengi wanapata kipato kidogo kwa sababu, hawatumii mbegu kuzalisha chakula, bali wanatumia nafaka.

Wataalamu hao walisema, unapotumia mbegu ya dukani kwenye kilimo unakuwa umejiweka katika asilimia 40 ya kupata kipato kikubwa, lakini desturi za wakulima wengi nchini na hata kupata kipato kidogo ni kutokana na wengi wao kugeuza nafaka kuwa mbegu.

Ni utaratibu wa kawadia tu, unakuta mkulima wa mahindi kutumia aliyoyavuna kama mbegu jambo ambalo walikosoa wataalamu hao wakidai ni kosa na linamfanya mkulima apate kipato kidogo.

Vilevile nimeshuhudia wakulima wa nyanya nao wanapovuna wanakamua mbegu ambayo wanakuja tena kuitumia kwenye msimu unaofuata wa kilimo jambo ambalo ni kosa kwa mujibu wa wataalamu hao.

Ni ukweli usiopingika, ili kupata kipato bora na mafanikio makubwa katika kilimo, inapaswa mkulima anunue mbegu kutoka dukani na sio kutumia mbegu inayotokana na mazao anayovuna, na itasaidia kupata uhakika wa kipato kikubwa na kujiondoa katika kilimo cha kujikimu na kufikia adhma ya kilimo biashara.

Pamoja na yote, unapojaribu kuwadodosa wakulima, nini huwa kinawakwamisha kufikia hatua hiyo huitaja gharama ya mbegu isiyotokana na nafaka kuwa juu.

Ninachokiona ni ukweli, ukiangalia kwa mfano mbegu ya nyanya ya dukani inauzwa kwa gharama kubwa sana na ili ulime heka moja, lazima uwe na laki tatu kwa ajili ya manunuzi ya mbegu tu.

Lakini, ile ya kukamua ambayo ndio inakosolewa na wataalamnu wa kilimo, ukipimiwa ya elfu 50, unaweza kulima zaidi ya ekari moja, hii inaonyesha dhahiri wakulima wanashindwa kwa sababu ya bei.

Ninachoishauri serikali na wadau wa kilimo, waweke utaratibu wa kuwakopesha wakulima mbegu bora, ili baada ya mavuno waweze kurejesha fedha zao. Hii itasaidia sana kwa wakulima ambao hawana uwezo wa kununua mbegu bora dukani.

Pia, kuwatembelea wanapokuwa shambani kuona maendeleo ya mazao yao na hata kuwasaidia pale wanapoona kuna shaka na uwezekano wa kupata kipato kikubwa kama kuwapatia mbolea na dawa kwa ajili ya tiba kwa mimea.

Suala la kuwapatia elimu sahihi juu ya utunzanji wa mazao, pamoja na kuwasaidia namna ya kupata soko kutokana na kile wanachokipata kutoka shambani.

Pamoja na kwamba serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa wakulima, lakini bado kuna makundi hayaguswi moja kwa moja, hasa wale wakulima walioko vijijini, kwa kuwa wengi wao hawajajiunga katika vyama vya ushirika lakini kuna haja ya kuangalia namna ya kuweza kuyafikia makundi hayo.

Ninashauri, pia serikali iangalie namna ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji vijijini kwenye maeneo ambako kuna ardhi kubwa, lakini hakuna umwagiliaji, kwa sababu eneo lenye umwagiliaji ni rahisi mkulima kupata kipato kikubwa na sio cha kubahatisha kama kutegemea mvua.

Unakuta kijiji kipo sehemu fulani kina ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, lakini hakuna maji kwa ajili ya umwagiliaji kwa hiyo wanalazimika kutumia kilimo cha msimu mmoja tu, yaani kile cha kutegemea mvua jambo amabalo linarudisha nyuma juhudi za kuinua sekta ya kilimo na uchumi wa nchi.

# Wafanyabiashara nchini kupokea malipo kadi za American Express

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BENKI ya CRDB imetangaza ushirikiano na kampuni ya kimataifa ya malipo ya American Express utakaowezesha benki hiyo kupokea matumizi ya kadi za American Express katika mtandao wake.

Hatua hiyo inatajwa itapanua wigo wa huduma za malipo kwa wateja wenye kadi hizo pindi wanapotembelea nchini.

Ushirikiano huo ambao umekwenda sambamba na uzinduzi wa matumizi ya kadi za American Express katika mtandao wa Benki ya CRDB, ulitangazwa juzi katika hafla maalum iliyofanyika jijini hapa, mgeni rasmi akiwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela aliyepongeza hatua hiyo na kusema itasaidia kuvutia wageni wengi zaidi nchini. Uzinduzi wa matumizi ya kadi hiyo unawezesha wateja wenye kadi za American Express kutumia kadi zao kufanya malipo kwa urahisi katika sehemu mbalimbali za huduma nchini zenye vifaa vya malipo vya benki hiyo pamoja na malipo ya mtandaoni. Wateja pia wamewezeshwa kutoa fedha taslimu kwenye ATM zinazofanya kazi kwenye mtandao wa benki hiyo.

Tangu mwaka 2017, American Express imeongeza mara tatu zaidi ya maeneo ambayo yanaweza kukubali kadi zake. Kadi hizo sasa zinatumika katika maeneo milioni 80 duniani kote.

Kukubalika kwa matumizi ya kadi hizi nchini kutasaidia biashara zenye mfumo wa malipo wa Benki ya CRDB kuongeza wateja zaidi kutoka katika wigo mpana wa wateja wanaotumia kadi hizo sio tu kutoka Afrika bali duniani kote. Hii inajumuisha wageni na wateja wanaosafiri kwa ajili ya biashara, utalii au kutembelea marafiki na familia.

Akizunguzuma katika hafla hiyo Mkuu wa Mkoa wa Arusha alisema uzinduzi wa matumizi wa kadi hizo utapelekea mazingira rafiki ya kufanya miamala kwa rahisi na usalama kwa wageni wanaotembelea nchini na katika mtindo waliouzoea, jambo ambalo linawajengea imani na kuwafanya wawe na hamu ya kurejea nchini na hivyo kuchochea utalii zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema benki hiyo inafurahi kuwa mshirika wa American Express nchini na kuwaruhusu wageni wa kimataifa wenye kadi za American Express kutumia kadi zao nchini.

Nsekela alisema ushirikiano huo unawapa watalii na wafanyabiashara wa kigeni wanaokuja Tanzania chaguo zaidi katika malipo.

"Hivi karibuni tumeshuhudia kuimarika kwa sekta ya utalii kwa kiasi kikubwa jambo ambalo limepelekea idadi ya watalii kuongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na jitihada zinazofanywa na serikali katika kuitangaza nchi na vivutio vyake.

"Makubaliano yetu na American Express yatasaidia kuwapa wageni uzoefu bora wa malipo pindi wawapo nchini, lakini pia yatafungua fursa mpya za biashara na kukuza wafanyabiashara wetu," alisema Nsekela.

Briana Wilsey, Makamu wa Rais na Meneja Mkuu wa Masoko ya Ulaya, Mashariki ya Kati na Afrika American Express, alisema: "Tunafurahia leo (juzi) hii kupanua zaidi idadi ya maeneo ambayo kadi zetu za American Express zitakuwa zikiweza kufanya duniani kote. Ushirikiano huu na Benki ya CRDB unawapa chaguo kubwa la malipo kwa wateja wenye kadi zetu zaidi ya milioni 135 wanaotembelea Tanzania kwa ajili ya utalii na biashara." Hafla hiyo ya uzinduzi wa matumizi ya kadi za American Express ilihudhuriwa na taasisi na wafanyabiashara wanaopokea malipo kupitia mfumo wa malipo wa Benki ya CRDB ikiwamo TANAPA, kampuni za utalii na Umoja wa Waongoza Watalii nchini (TTGA).




Mjumbe kutoka Api-support Dk. Dastan Kabialo akiwasilisha mada kwa washiriki wa mjadala wa namna ya kurahisisha taratibu za usafirishaji wa bidhaa za asali kwenda nje ya nchi wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na Shirika la Kimataifa la Biashara (ITC), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Mjadala huo, ulihusisha taasisi na mashirika muhimu ya umma kama vile TBS, TRA, TanTrade, TIC, TCCIA na CCM ikiwa ni sehemu ya Mradi wa Kuchangia Mnyororo wa Thamani wa Ufugaji Nyuki (BEVAC) unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Balozi nyumba 10 adaiwa kuwakata vidole watuhumiwa wizi wa nondo

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

BALOZI wa Shina namba 10 Mji Mwema, Samuel Mtambo, Mkazi wa Mtaa wa Nasele katika kata ya Mpemba, Wilayani Momba, anashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Songwe kwa tuhuma za kuwakata vidole vya miguu vijana wawili wa familia moja.

Inadaiwa kuwa kiongozi huyo kwa kushirikiana na wakazi wengine wa eneo hilo, walitenda ukatili huo baada ya kuwakamata vijana hao na vipande 17 vya nondo wanavyodaiwa kuviiba kwenye moja ya nyumba katika mtaa wa balozi huyo.

Mtuhumiwa huyo na wenzake wawili ambao wanaendelea kutafutwa na jeshi hilo, wanadaiwa kuwakata vidole vijana hao; Zefania Mdollo (20) na Kelvin Mdollo (17) kwa kutumia msumeno unaodaiwa kutumiwa na vijana hao kukata vipande vya nondo wanazotuhumiwa kuiba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu tukio hilo, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya kufanya tukio hilo la ukatili alilolitenda kwa kushirikiana na wenzake wawili Novemba 3, mwaka huu.

"Inasemekana kwamba vijana hawa ambao ni ndugu walifika kwenye nyumba ambayo inajengwa na tayari imewekwa nondo na kuanza kukata vipande vya nondo ndipo walipokamatwa na mtuhumiwa (balozi) akiwa na wenzake wawili na kuchukua msumeno uliotumiwa na vijana hao na kuwakata vidole vya miguu," alisema.

Kamanda Mallya alisema kijana Zefania alikatwa kidole kikubwa cha mguu wa kushoto huku mdogo wake akikatwa kidole cha mguu wa kulia.

Alibainisha kuwa baada ya kutendwa ukatili huo, walitoa taarifa Kituo cha Polisi Mpemba kwa kuandikisha majina ya uongo, kwa kuwa walijua walifanyiwa ukatili huo baada ya kukutwa wanaiba nondo.

Alisema kuwa baada ya kutoa taarifa katika kituo hicho cha polisi na kupatiwa fomu namba tatu ya polisi (PF3) kwa ajili ya matibabu, vijana hao hawakwenda kupatiwa matibabu hospitalini badala yake waliendelea kujiuguza kwa kificho hadi jeshi hilo lilipopata taarifa na kufanikiwa kumkamata mtuhumiwa.

Kamanda Mallya alisema kuwa baada ya vijana hao kukamatwa, wanaendelea kupatiwa matibabu kwa usimamizi wa jeshi hilo.

# Kampuni ya uwakili yajivunia kuwezesha kutungwa sheria

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya Uwakili ya IMMMA Advocates, imesema kwa miaka 26 tangu kuasisiwa kwake, inajivunia kutoa elimu na msaada wa kisheria kwa jamii na kuwezesha upatikanaji sheria kadhaa nchini na nje ya nchi.

Imesema mbali na hilo, kwa kipindi hicho cha miongo miwili na nusu, pia imetoa mafunzo katika Shule Kuu ya Sheria mara tu ilipoanzishwa ikiwa na uhaba wa wakufunzi pamoja na kushirikiana na serikali kupatikana miradi ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Protase Ishengoma, mwanzilishi mwenza wa kampuni hiyo, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari akielezea mafanikio na changamoto walizopitia, huku mwenyewe akistaafu.

"IMMMA Advocates imefanikisha upatikanaji wa PPP hapa Tanzania na Ghana. Tumefanikisha kupatikana kwa mkataba wa pamoja wenye manufaa kwa kushirikiana na serikali ya Somalia," alisema Ishengoma.

Alikumbusha kuwa kampuni hiyo pia imefanikisha kuwafunza na kufanikisha ndoto za wanasheria kadhaa nchini, ambao kwa sasa ni majaji na mawakili kwenye taasisi tofauti ndani na nje ya nchi.

"Tunajivunia kufanya marekebisho ya Sheria ya Kampuni ya Mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Nishati na Sera ya Nishati Zanzibar.

Pia wakati mifuko ya hifadhi ya jamii inaungana, kulihitajika utengamano wa kisheria kwa maana mali na uwekezaji wa wanachama," alikumbusha Ishengoma.

Sadock Magai, mwanzilishi mwenza wa kampuni hiyo, alisema wakati mmoja wao akistaafu, ataendelea kukumbukwa kutokana na mchango wake alioutoa ikiwamo kutoa msaada wa kisheria kwa jamii.

Alisema kampuni hiyo hushirikiana na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kufanikisha utetezi wa kisheria kwa masuala ya haki husasan kwa wanawake na watoto.

"(Ishengoma) uliweza kufika Zambia katika magereza na kutoa msaada wa kisheria kwa wafungwa hasa watoto, na ilisaidia baadhi yao kutoka kifungoni kwa kuwa wengine walikuwa hawana uelewa wowote kuhusu sheria na hata fedha," alisema.

Akizungumzia mafunzo kwa wanasheria katika Shule Kuu ya Sheria, Magai alisema kampuni yao iliwezesha wadau wao wa ndani na nje ya nchi kutoa elimu bila malipo na hata kuwezesha wataalamu wa nje kuja kufundisha shuleni huko, akibainisha baadhi yao hulipwa hadi dola za Marekani 4,000 kwa saa.

"Wenzetu kutoka nje walikuja nchini kuoa mafunzio bure kutokana na ubia wetu kati yao. Ikumbukwe wakati Shule Kuu ya Sheria ilipoanza hakukuwa na wataalamu wa kutosha kutoa mafunzo," alisema Magai.

Kampuni ya IMMMA Advocates ilianzishwa mwaka 1997 na Ishengoma, Magai, Lawrence Masha na Aloysius Mujulizi kwa lengo la kutoa huduma ya kisheria.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

# MWITO WA KUTOA MAONI

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba leseni kujihusisha na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni | Aina ya Ombi la Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Brava Energy Ltd - Kigoma Petrol Station S.L.P 4625, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 153/3, Eneo la Kigoma/Ujiji, Wilaya ya Kigoma, Mkoa wa Kigoma. | Ahmed Ali Mohamed (Mkenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 2. | Asamoil Company Limited S.L.P 15730, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 19 & 20, Eneo la Kumsenga, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. | Azhad Soud Suleiman (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 3. | Charles Stephano Mahalage, S.L.P 113, Shinyanga. | Kiwanja Na. 4, Kitalu “A”, Eneo la Mwakitolyo, Wilaya ya Shinyanga, ,Mkoa wa Shinyanga. | Charles Stephano Mahalage (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 4. | Oryx Energies Tanzania Limited - Nzega Service Station S. L. P 9540, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 23 na 24, Kitalu “B”, Eneo la Nzega Mjini, Wilaya ya Nzega, Mkoa wa Tabora. | Kalpesh Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 5. | Ipyana Watson Mwakatenya S. L. P 23, Mwadui | Eneo la Viwandani,Wilaya ya Shinyanga Mkoa wa Shinyanga. | Ipyana Watson Mwakatenya (Mtanzania) | Leseni ya Usabazaji wa Gesi ya Kupikia Majumbani (LPG) | Ombi la Leseni Mpya |
| 6. | Olympic Petroleum (T) Limited - Kasulu S.L.P 6185, Mwanza | Kiwanja Na.202 Kitalu “O” Eneo la Kasulu Mjini, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. | Ally M. Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 7. | NGS Petroleum Limited-Majimoto S. L. P 20, Bariadi | Kiwanja Na. 1, Kitalu “C”, Eneo la Majimoto, Wilaya ya Mlele, Mkoa wa Katavi. | Njalu Daudi Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 8. | Brava Energy Limited S.L.P 4625, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 8, Kitalu “C”, Eneo la Shunu, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga. | Ahmed Ali Mohamed (Mkenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 9. | Fast Energies Solution Limited S. L. P 475, Kasulu | Kiwanja Na. 179, Kitalu “N”, Eneo la Kasulu Mjini, Wilaya ya Kasulu, Mkoa wa Kigoma. | Twallybu Yasin Ismaily (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 10. | Jambo Petroleum Products Ltd, S. L. P 71, Shinyanga | Kiwanja Na. 1909, Kitalu “NN”, Eneo la Ibadakuli, Wilaya ya Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga. | Seleman Khamis Al-Amri (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 11. | Ng'wanaibengwe Agro-Vet Company Limited, S. L. P 342, Kahama. | Kiwanja Na. 1255, Kitalu “B”, Eneo la Wigehe, Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga. | Yahya Ramadhan Bundala (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 12. | Chief Mwampulo Company Limited, S. L. P 7281, Kahama. | Kiwanja Na. 3, Kitalu “A”, Eneo la Bunango, Wilaya ya Msalala, Mkoa wa Shinyanga. | Mwampulo Davis Kamwisile (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 13. | Olympic Petroleum(T) Limited, S.L.P. 6185, Mwanza. | Kiwanja Na. 258, Kitalu “J” Eneo la Nyamanoro, Manispaa ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza | Ally Mohamud Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 14. | Brava Energy Limited, S. L. P. 4625, Dar es Salaam | Eneo la Runzewe, Wilaya ya Bukombe, Mkoa wa Geita. | Ahmed Ali Mohamed (Mkenya) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 15. | Manyanyas Oil Limited, S.L.P 132, Tunduma. | Kiwanja Na. 1, Kitalu “B”, Kakozi -Ndalambo, Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe | Bahati Msajie Mnozya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 16. | Oryx Energies Tanzania Limited, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 57, Kitalu “F”, Vwawa Mjini, Wilaya ya Mbozi, Mkoa wa Songwe. | Kalpesh Mehta (Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 17. | Oryx Energies Tanzania Limited, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Barabara ya Tanzam Highway, Wilaya ya Makambako Mjini, Mkoa wa Njombe | Kalpesh Mehta (Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 18. | Oryx Energies Tanzania Limited, S.L.P 9540, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 60, Kitalu “I”, Tunduma Mjini, Wilaya ya Momba, Mkoa wa Songwe | Kalpesh Mehta (Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 19. | Oryx Energies Tanzania Limited, S.L.P 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Likuyufusi, Peramiho, Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma | Kalpesh Mehta (Uingereza) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 20. | Ntanyinya Petrol Station, S.L.P 101, Chunya. | Kiwanja Na. 30, Kitalu “O”, Kabwe – Mwanjelwa, Jiji la Mbeya, Mkoa wa Mbeya | Fidelis Alphonce Ntanyinya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 21. | Ntanyinya Petrol Station, S.L.P 101, Chunya. | Kiwanja Na. 328, Kitalu “B”, Kongolomkola, Mswiswi, Wilaya ya Mbarali, Mkoa wa Mbeya. | Fidelis Alphonce Ntanyinya (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 22. | Oryx Energies Tanzania Limited - Great North Ss, S.L.P. 9540, Dar es Salaam. | Kiwanja No. 791/11/1, Kitalu “E”, Eneo la Ipogolo, Wilaya ya Iringa Mjini, Mkoa wa Iringa. | Kalpesh Mehta (Mwingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 23. | Zauda Shaban Dodi T/A Kinyasi Filling Station, S.L.P. 11, Kondoa. | Kiwanja No. 81/KDC/3, Eneo la Kijiji cha Kinyasi, Kata ya Kinyasi, Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. | Zauda Shabani Dodi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 24. | Landmark Filling Station Limited, S.L.P. 64, Kongwa. | Kiwanja No. 109, Kitalu “F”, Eneo la Kongwa, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma | Job Yuston Ndugai (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 25. | Njombe Filling Station Company Ltd.-Dodoma, S.L.P. 411, Njombe. | Kiwanja No. 65, Kitalu “R”, Eneo la Chadulu, Wilaya ya Kongwa, Kata ya Makole, Wilaya ya Dodoma Mjini, Mkoa wa Dodoma. | James Malika Mwinuka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 26. | Mohamedi Hussein Mohamedi Songambele, S.L.P. 103, Kibaya. | Eneo la Kijiji cha Songambele, Wilaya ya Kongwa, Mkoa wa Dodoma. | Mohamedi Hussein Mohamedi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 27. | Mogas Tanzania Ltd, S.L.P 70284, Dar es Salaam. | Barabara ya Bandari, eneo la viwanda-Kurasini Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Emmanuel Nkya (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya vilainishi | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 28. | Rogas E.A Limited S.L.P 75564, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P5353 na P5355, Eneo la Mbagala Kuu, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Rehema Hamza Chegeka (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 29. | Africa Energy Ltd S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 130, Kitalu ‘A’, Eneo la Manzese, Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 30. | GBP Tanzania Limted-Port Service Station, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja na. P17265, Eneo la Kurasini, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 31. | Vel Estate Company Ltd, S.L.P. 56314, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 257, 259 and 261, Kitalu “E”, Eneo la Tegeta, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Vincent Lyimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |

217748002

# TANGAZO


| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Leseni | Aina ya Ombi la Leseni |
|---|---|---|---|---|---|
| 32. | VIVO Energy Tanzania Ltd, S.L.P. 78470, Dar es Salaam. | Shamba na. 1031, Kijiji cha Sango, Manispaa ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 33. | National Oil Tanzania Limited-Mbagala Service Station, S.L.P. 70048, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 21, Eneo la viwanda la Mbagala, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Moteza Augustine Mushi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 34. | VIVO Energy Tanzania Ltd, S.L.P. 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 5, Eneo la Ubungo, Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar es Salaam. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 35. | Barrel Petro Energy Co. Ltd-Mikocheni Service Station, S.L.P. 21420, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 411, Eneo la Mikocheni, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Khalid Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 36. | Lake Oil Ltd-Bunju Petrol Station, S.L.P. 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 83, Kitalu "A", Eneo la Bunju, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Allyu Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 37. | Puma Ocean Road Service Station, S.L.P. 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 2107/5, Eneo la Ocean Road, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Fatma Abdalah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 38. | Amos Site Mabena T/A Mabena Petrol Station, S.L.P. 710, Songea. | Kiwanja na. 29, Eneo la Kongowe, Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani. | Amos Site Mabena (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 39. | Acer Petroleum (T) Ltd-Nachingwea, S.L.P. 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 843, Kitalu "J", Eneo la Pachani, Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi. | Atul Mittal (Mtanzania | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 40. | VIVO Energy Tanzania Ltd, S.L.P. 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 182, Kitalu "C", Wilaya ya Nanyamba, Mkoa wa Mtwara. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 41. | Olympic Petroleum Ltd-Tabata Segerea, S.L.P. 16484, Dar es Salaam. | Kiwanja na. P28250, Eneo la Tabata Segerea, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Ally Adon (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 42. | Puma Sam Nujoma Service Station, S.L.P. 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 1, Kitalu "C", Eneo la Viwanda, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Fatma Abdalah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 43. | Epsom Energy Tanzania Limited, S.L.P. 76500, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 81, Eneo la Regent Estate, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Herbert Okundi Omune (MKenya) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 44. | GSG Oil Company Limited, S.L.P. 76500, Dar es Salaam | Eneo la Mikocheni, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Mwajuma Salim Choggy (Mtanzania) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 45. | Tosha Petroleum Tanzania Limited, S.L.P. 31113, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 6, Kitalu "G", jengo la NSSF Mwalimu Nyerere, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Abdisirat Khalif Ali Nur (Mkenya) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 46. | Yas Oil Company Limited, S.L.P. 4804, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 74, Kitalu "M", Eneo la Kariakoo, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Yasir Abdallah Saleh (Mtanzania) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 47. | Ayoun Trading Limited S.L.P. 21279, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 235, Eneo la Oysterbay, Manispaa ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Jaweed Moosa Patel (Mtanzania) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 48. | Keda (Tanzania) Ceramics Company Limited, S.L.P. 81, Pwani. | Kiwanja na. 1,2,3,4,5,6 & 7, eneo la Msufini, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani. | Zhang Wan (Mchina) | Leseni ya kituo kwa matumizi binafsi | Ombi la Leseni Mpya |
| 49. | Mogas Tanzania Ltd, S.L.P. 70284, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 310/3, eneo la Kurasini, Wilaya ya Temeke, Mkoa wa Dar es Salaam. | Emmanuel Nkya (Mtanzania) | Leseni ya jumla ya vilainishi | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 50. | Mana Company Ltd S.L.P. 66660, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 2/1, eneo la Tegeta, Wilaya ya Kinondoni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Nabahan Salim Kadari (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 51. | Redav Exraw Company Limited-Msolwa, S.L.P 42445, Pwani. | Kiwanja na. 1, Kitalu "G", eneo la Msolwa, Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani. | Evans David Masumbigana (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 52. | Bil Energy Company Ltd S.L.P 42577, Pwani. | Kiwanja na. 1, Kitalu "G", Eneo la Chamakweza, Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani. | Abdulrahman Ahmed Hassan (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 53. | Yusuph Amani Maimu, S.L.P. 90005, Dar es Salaam. | Kiwanja na. 20, Kitalu "CC", eneo la Chanika, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. | Yusuph Amani Maimu (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 54. | Oil Link (T) Limited S.L.P. 106093, Dar es Salaam. | Kiwanja na. P13493, Eneo la Tungi, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Aref Abdallah Bakhamis (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 55. | Overland Petroleum Company Limited, S.L.P. 505, Dar es Salaam. | Kiwanja 39, eneo la Keko, Manispaa ya Temeke, Mkoa wa Pwani. | Faisal Awadh (Mtanzania) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 56. | Fountain Petroleum Ltd, S.L.P. 826, Mtwara. | Kiwanja na. 247, kitalu "C", eneo la Ufukoni, Manispaa | Mehboob Osman (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| | | ya Mtwara, Mkoa wa Mtwara. | | | |
| 57. | Delvin Transportation and Supply, S.L.P. 100246, Dar es Salaam. | Kijiji cha Vianzi, Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani. | David Jackson Massam (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 58. | FMS Oil Company Ltd S.L.P. 67089, Dar es Salaam. | Eneo la Toangoma, Manispaa ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam. | Faraj Mbarak Binkleeb (Mtanzania) | Leseni ya jumla Mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 59. | Lukase Company Limited, S.L.P 703, Moshi – Kilimanjaro. | Kiwanja namba 1, Eneo la Mgagao, Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro. | Raston Josephat Gabusha (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 60. | Vivo Energy Tanzania Limited - Tengeru Petrol station, S.L.P 78470, Dar es salaam. | Shamba namba 2261, Kijiji cha Moivaro, Wilaya ya Meru, Mkoa wa Arusha. | Emmanuel Steven Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 61. | Vivo Energy Tanzania Limited - Segera Petrol station, S.L.P 78470, Dar es salaam. | Kiwanja cha 3/2/2, Kitalu "V", Eneo la Segera, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga. | Emmanuel Steven Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 62. | Olasiti Investment Ltd – Mirongoine Petrol station, S.L.P 10275, Arusha. | Kijiji cha Mirongoine, Kata ya Oljoro, Wilaya ya Arusha vijijini, Mkoa wa Arusha. | Innocent Simon Moshi (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi Jipya La Leseni |
| 63. | Kimweri Oil & Filling Station Ltd, S.L.P 86, Hedaru – Same, Kilimanjaro. | Kiwanja namba. HAD/339, Eneo la Hedaru, Wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro. | Twaha Francis Kimweri (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 64. | Masry Energy Co. Ltd, S.L.P 400, Babati – Manyara. | Kiwanja namba 80 na 81, Kitalu "B", Kijiji cha Gallapo , Wilaya ya Babati , Mkoa wa Manyara. | Abdallah S. Athumani (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 65. | Sango Petrol Station – Mto wa Mbu petrol station, S.L.P 919, Moshi – Kilimanjaro. | Kiwanja namba 1973, Eneo la Mto wa Mbu, Wilaya ya Monduli, Mkoa wa Arusha. | Irene Wilfred Tarimo (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 66. | Great North Service Station Ltd – West Meru, S.L.P 12318, Arusha. | Kiwanja namba 66, Kitalu "C",Eneo la Biashara West Meru, Wilaya ya Arumeru , Mkoa wa Arusha. | Robson Elishilia Laseko (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 67. | Admire Oil Limited – Namanga Petrol station, S.L.P 7494, Dar es salaam. | Kiwanja namba 46 & 47, Kitalu "C", Eneo la Namanga, Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 68. | Lake Oil Limited – Chumbageni Petrol station, | Kiwanja namba 671/16, Kitalu" KBV", Eneo la | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya rejareja ya mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| | S.L.P 5055, Dar es salaam. | Chumbageni, Halmashauri ya jiji la Tanga mjini, Mkoa wa Tanga. | | | |
| 69. | Kuringe Transport Company Limited, S.L.P 50, Sanya Juu. | Kiwanja Namba 7, Kitalu "E", Eneo la Longido Mjini, Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha. | Liberatus Silvester Temu (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 70. | Shabani Selemani Mfinanga, S.L.P 13, Himo. | Kiwanja Namba 201, Kitalu "H", Eneo la Himo, Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro. | Shabani Selemani Mfinanga (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Leseni Mpya |
| 71. | Vivo Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es salaam. | Kiwanja Namba 62, Kitalu "DD", Eneo la Mianzini, Halmashauri ya Jiji la Arusha, Wilaya ya Arusha Mjini, Mkoa wa Arusha. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 72. | TSN Oil (T) Ltd – Mkinga S.L.P 12288, Dar es salaam. | Kiwanja Namba 29, Kitalu "C", Eneo la Kasera, Kata ya Mkinga, Willaya ya Mkinga, Mkoa wa Tanga. | Ahmed M. Baghozah (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 73. | Great North Service Station Limited – West Meru, S.L.P 12318, Arusha. | Kiwanja Namba 66, Kitalu "C", Eneo la West Meru, Wilaya ya Arumeru, Mkoa wa Arusha. | Robson Elishilia Laseko (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 74. | Acer Petroleum (T) Ltd, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Shamba Na. 1320 & 1321, Kibisi, Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Mbeya. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |
| 75. | Acer Petroleum (T) Ltd, S.L.P 78845, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5, Kitalu "K", Uyaoni, Wilaya ya Namtumbo Mjini, Mkoa wa Ruvuma. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta | Ombi la Kuhuisha Leseni |

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote wa leseni hapo juu kwamba asipewe leseni, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go.tz

217748002





# Makalla aagiza mkandarasi barabara ya Sengerema-Nyehunge aondolewe

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amewasilisha ombi kwa Wizara ya Ujenzi kusitisha mkataba na Mkandarasi AVM-Dillingham Costruction International waliyeingia naye Mkataba wa ujenzi wa barabara ya Sengerema-Nyehunge baada ya kushindwa kuanza kazi hiyo katika muda uliopangwa.

Serikali ilisaini Mkataba wa ujenzi wa barabara hiyo Aprili, mwaka huu yenye urefu wa Km 54.4 ikigharimu Sh.bilioni 73.47 huku mkandarasi akitakiwa kuanza kazi hiyo mwezi Agosti lakini mpaka sasa bado hajaanza utekelezaji wake.

Makalla amesema hayo jana wakati wa ufunguzi wa kikao cha kwanza cha Bodi ya Barabara ya Mkoa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kuagiza Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) kuandika barua ya kutokuridhishwa na mkandarasi huyo ili aletwe mwingine.

"Huyu Mkandarasi alitakiwa kuwa kazini mwezi wa nane akaongeza muda mpaka wa kumi lakini mpaka sasa mwezi wa kumi na mbili hakuna chochote alichokifanya pia nina taarifa zake kuwa hata Mbeya amechukua mradi na bado hajaanza, hatufai kabisa," "Hii ndiyo shida ya makandarasi kuomba miradi kwa gharama ndogo na kuzitangaza kampuni zao kuwa kubwa na zenye uwezo kumbe kazi hawawezi, cha kushangaza hii ni kampuni ya nje na imehitaji malipo ya awali sasa si ni bora kumtumia tu mkandarasi wa ndani,"alisisitiza RC Makalla

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa TANROADS Mkoa wa Mwanza, Mejea wa wakala huo Mkoa, Mhandisi Pascal Ambrose, alisema mpaka sasa mkoa una jumla ya barabara kuu za Mkoa na Wilaya km 1,145.50 ambapo kiwango cha lami ni km 294.16 na changarawe 851.34 huku wakikasimu jumla ya barabara za wilaya za kiwango cha changarawe km 202.18.

"Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 tumekamilisha barabara za Ibanda na Mwanza-Shinyanga kwa zaidi ya Sh.bilioni 3.1 na miradi mingine ya barabara pamoja na madaraja likiwemo daraja la JPM ambalo kwa sasa lipo katika hatua za mwisho,"alisema Mhandisi Ambrose.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Mwanza Mhandisi, Makori Kisale, alisema halmashauri zote zina mtandao wa barabara kwa jumla Km 8586.763 mpaka kufikia Juni, mwaka huu.

Alisema kati ya hizo barabara zilizopo kwa kiwango cha lami ni Km 99.892,Changarawe ni Km 1,797.785,barabara za udongo Km 6,659.008, Zege km 11.339 na mawe km 18.739.



Ofisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Manispaa ya Kahama, Richard Hegera (katikati) na wafanyakazi wa Barrick wakiangalia maendeleo ya mradi wa ufugaji kuku wa mayai kabla ya mgodi huo kuukabidhi kwa kikundi cha wanawake cha Busabi, Kahama jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC Mndeme ashtushwa ubovu wa barabara Ibanza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, ameshtushwa na hali ya ubovu wa barabara katika Kijiji cha Ibanza, Kata ya Mwamala, wilayani Shinyanga kilichokumbwa na Mvua za Mawe na upepo mkali na kusababisha nyumba 51 kuanguka, majeruhi na mashamba kuharibiwa.

Kufuatia ubovu wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa mbili Mndeme alimwagiza Wakala wa Barabara Mjini na Vijijini (TARURA) wilayani Shinyanga kuanza ukarabati haraka iwezekanavyo.

Diwani wa Kata ya Mwamala, Hamisi Masanja, alisema wananchi wamekuwa wakipata shida kuzunguka katika barabara kuu kufika mjini Shinyanga umbali wa Kilomita 20, lakini barabara hiyo ikitengemaa watatumia kilomita 2 tu.

"Mfano majeruhi wa mvua hii ya mawe na upepo imetuchukua muda mrefu kuwakimbiza Hospitali ya Rufani kwa kuzunguka katika barabara kuu na tungetumia barabara hii safari ingekuwa ya haraka na mapema,"alisema Masanja.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Shinyanga Mhandisi Samson Pamphil, alisema tayari barabara hiyo ipo kwenye bajeti ya matengenezo na wanachosubiri ni mkandarasi kutia saini na kuanza kazi.

Aidha serikali imesema itagharimia matibabu ya majeruhi wote wa tukio hilo akiwemo bibi ambaye alivunjika mguu baada ya kupondwa na tofali.

# Diwani alalamikia mradi wa maji kuchelewa kukamilika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

DIWANI wa Kata ya Busangi Halmashauri ya Msalala, Alixander Mihayo amelalamikia shughuli za utekelezaji wa mradi wa maji wa Nduku-Busangi kuchukua muda mrefu kukamilika licha ya kubadilishiwa makandarasi mara mbili na kusababisha wananchi kuchelewa kupata huduma.

Mihayo alitoa malalamiko hayo juzi kufuatia ziara ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maji mkoani Shinyanga wakiambatana na Mbunge wa Viti Maalum Santiela Kirumba pamoja na Mbunge wa Jimbo la Msalala, Iddi Kassimu.

Alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Julai, 2020 na walitaarifiwa kuwa awamu ya kwanza imekamilika lakini hakuna maji yanayotoka huku wananchi bado wanatumia maji yasiyo safi na salama.

"Endapo mradi huo utasimamiwa vema na kuanza kutoa huduma utasaidia kuwaondolea adha wananchi ya kutumia maji machafu ikiwemo kutembea umbali mrefu kutafuta maji, kwani wanaohangaika na hilo ni wanawake na wanafunzi hasa wa kike,"alisema Mihayo.

Akijibu malalamiko hayo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Kahama, Paschal Mnyeti, alisema ujenzi wa mradi wa maji Nduku-Busangi-Nyamigege, utakuwa na tangi lenye mita za ujazo 100,000 na vituo 16 vya kuchotea maji na vimekamilika kwa asilimia 97.

Kuhusu kuchelewa kukamilika Mnyeti alikiri tatizo na kutaja sababu za kuwa ni kukosekana kwa mabomba ya chuma kwa wakati lakini kwa sasa yamepatikana na awamu ya pili ya mradi itakamilika mwezi Julai 2024 na kila Kijiji kitapata maji hayo.

Mbunge wa Jimbo hilo, Iddi Kassimu, aliwaondoa hofu wananchi juu ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama na kusema kuwa jimbo hilo limepokea zaidi ya Sh.bilioni 12 kwa ajili ya kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kwa uhakika.


Alisema ujenzi wa miradi hiyo unaendelea katika maeneo ya vijiji vya Mwazimba, Mwashigini, Buyange, Ilogi, Bulyanhulu na Kata ya Ikinda hivyo kila mwananchi atafikiwa na maji safi.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Shinyanga, Santiel Kirumba alisema, serikali imekuwa ikishirikiana na wadau wa maendeleo kutatua tatizo la maji vijijini, sasa maeneo mengi nchini kuna maji safi na salama na kwa asilimia kubwa.



Ukurasa 14

MAZITO SEMINA ZA TGNP INAYOYAIBUA...
Unyama jinsia mitaani unavyozaa shida afya, umasikini na kasoro kupata sheria




**Jamani tujipange, kipindupindu kimeua Kagera, nasi tukae mkao wa tahadhari**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA DESEMBA 8, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

WAJIBU WA MATAIFA TAJIRI…

# Kikao cha COP 28 chajibu rai ya Samia kikao kama hicho Scotland

## •Shida 'mama na mtoto' uhalisia waonekana Katesh

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA safari zake kiuchumi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan daima anaunganisha njia za kiuchumi, katika ubia na mazingira kuwa 'chanda na pete', kwa maana zinategemeana kwa mafanikio, hata athari, mfano hai ukiwa katika sekta za kilimo na uvuvi.

Upande wa kimataifa, tangu kuingia kwake katika nafasi ya sasa amekuwa mvuto, kuanzia katika mikutano ya jirani kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, zingine Afrika na hata ughaibuni kimataifa; anaanika hoja katika uchumi na mazingira .

Hilo ndilo linalotawala katika 'eneo lake la kujidai', mikutano ya COP ambako mzizi wake ana asili nayo. Akiwa na miezi tisa kazini, Rais Dk. Samia mnamo Novemba 2021, katika mkutano wa 26 kuhusu mabadiliko ya tabianchi, Glasgow nchini Scotland, akatoa wito maalum kupitia hotuba yake.

Hapo akasisitiza kwamba juhudi za pamoja zinahitajika kukabili athari za mabadiliko hayo, kwani hazichagui nchi zilizoendelea au zinazoendelea.

Akatumia mfano wa Tanzania, mabadiliko ya tabianchi yanavyoathiri ardhi ya uzalishaji mali, kina cha bahari, kuyeyuka kwa barafu kilele cha Mlima Kilimanjaro, huku visiwa vya Zanzibar vikiathirika na ongezeko la joto linalotegua ikolojia inayovutia watalii.

Anafafanua hayo yanatokea, licha ya serikali kuendelea na azma yake kutenga hekta milioni 48 kwa ajili ya utunzaji misitu, hivyo akataja mkakati kupunguza athari za hewa ukaa kwa asilimia kati ya 30 na 35 ifikapo mwaka 2030.



Rais Samia alipokuwa kwenye kikao cha COP 26, nchini Scotland. **PICHA: MTANDAO**

Hayo yote ni pesa, hapo ndipo Dk. Samia, anaelekeza rai yake kwa nchi zilizoendelea kutimiza ahadi zao kuratibu upatikanaji wa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 100, kwa ajili ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi hususan kwa nchi zinazoendelea.

Vivyo hivyo, katika kikao cha pembeni cha wanawake viongozi katika mjumuiko huo wa jijini Glasgow, pia Rais Dk. Samia, akahutubia akiainisha namna athari hizo zinavyomgusa mwanamama na mtoto.

Mwaka unaofuata, Dk. Samia katika hadhi yake ilele, mwenyeji wa hotuba zinazotoa mwelekeo, katika mkutano wa Cop uliofanyika nchini Misri, Novemba mwaka jana na mwaka huu, uko unaendelea Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu nako akapewa kipaza sauti kuhutubia dhana yenye pacha tatu 'mazingira, jamii na uchumi.'

Kama ilivyo kawaida yake, mbali na kupewa nafasi ya kuhutubia, ikaendana na majibu alipoyaambia mataifa makubwa zipatikane Dola za Marekani Bilioni 100 za kukabili mazingira, wiki iliyopita mkutanoni Dubai, kukatangazwa kutolewa sehemu ya fedha hizo.

Hicho ni kiasi cha Dola za Marekani milioni 400 zimetolewa na mataifa makubwa kama Marekani, Umoja wa Ulaya (EU), pia Uingereza, taswira ikionyesha namna sauti ya mkuu huyo wa nchi ina nguvu, zaidi ya hapo wadau wengine wakiwamo wenyeji, Umoja wa Falme za Kiarabu nao kutangaza ofa.

Hata hivyo, Dk. Samia amelazimika kukatisha mahudhurio yake ya mkutano safari hii, akikimbilia nyumbani kuhani na kusaidia maafa yaliyotokea maporomoko yatokanayo na volkano, huko Katesh, Hanang, ambako jana alishawasili huko.

Picha pana ya yaliyotokea huko Katesh, yanaendana na majibu yaliyoko katika hotuba mbili za Rais Dk. Samia katika mkuano wa COP huko, Glasgow, Scotland.

Eneo la kwanza, linajibiwa na namna nchi zilizoendelea ndani ya miaka miwili tangu rai hiyo kutolewa, zimejibu kwa kuchangia jumla ya Dola za Marekani milioni 400, ambayo ni sawa na asilimia 40 ya ombi lake Dk. Samia.

Vilevile, akiwa kwenye kikao cha viongozi wanawake, huko nchini Scotalad, uchambuzi wake ni kuhusu kinamama na Watoto, ndio sasa kinashuhudiwa huko Katesh, ambako katika wastani wa waliofariki 68, hadi juzi jioni, theluthi mbili ni kinamama na watoto.

**TANZANIA ILIVYOJIPANGA**

Ujumbe wa Tanzania mkutanoni Dubai, ulipangwa kushirikisha mawaziri, makatibu wakuu, mabalozi, viongozi na wataalamu kutoka wizara za kisekta, idara za serikali, mashirika ya umma, vyuo vikuu, sekta binafsi, asasi za kiraia, vijana na wanahabari wa pande mbili za muungano.

Kikao hicho ambacho kinaendelea, wanaohudhuria matarajio yalikuwa washiriki zaidi ya 70,000 kutoka nchi takribani 190.

Hapo ni safu inayojumuisha wakuu wa nchi na serikali wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi wanaohutubia mkutano, Dk. Samia akiwa mzungumzaji wa 11, kati ya wakuu 160 wanaoshiriki mkutanoni.

Pia, Tanzania ikatarajiwa kuwa mwenyeji wa mikutano mikuu mitatu ya pembezoni inayohusu Nishati Safi ya Kupikia, Kilimo Endelevu, na Uchumi wa Buluu.

Katika Mkutano unaohusu nishati safi ya kupikia, Rais alipangiwa kuongoza wenzake duniani, kuzindua Programu ya Kuwakomboa Wanawake wa Afrika Kupitia Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia, maarufu 'African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP'.

UCHUMI

# Mradi Uvuvi ulivyoleta maisha mapya kwa wavuvi Victoria

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

NI zaidi ya nuru jua la siku nzima kugeuka historia, kazi kufanyika kwa saa 12 bila ya kutetereka. Sasa ni zamu ya wavuvi kutoka mwalo wa Igombe Kayenze ndogo wilayani Ilemela, vilio vyao vya kupoteza maisha kwa mlipuko wakiwa ziwani, dagaa kusombwa na maji ,kukosa ubora ,kushinda juani sasa basi.

Frank Faustine, mvuvi wa dagaa kwa zaidi ya miaka 15 akiieleza Nipashe adha walizokuwa wakikumbana nazo wakati wakitekeleza majukumu yao ya uvuvi wa dagaa Ziwa Victoria.

Anasema, kupoteza maisha wakiwa katika majukumu yao ni jambo la kawaida, akifafanua wanavyopoteza Maisha, taa za kuvua aina ya koroboi zinazotumia mafuta ya taa ndio chanzo kikuu, kwani kuna wakati zinalipuka na kusababisha ajali.

Ni mlipuko unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na mafuta ya petroli yanayoyatumika kuendesha mitubwi yao .

Pia, anaeleza kuwa koroboi hizo ni chanzo kikubwa cha madhara kwa viumbe majini, kwa sababu mwanga wake ulikwenda chini, hivyo ujio wa taa za nishati ya jua za kuvulia samaki na dagaa, sambamba na mtambo wa ukaushaji, ni ukombozi katika sekta yao.

Anataja nafuu nyingine, ni kwa viumbe majini mwanga wake unapiga pembeni kwa kusambaa na hazipigi kwenda chini sana.

Faustine anafafanua, kwa sasa wana uhakika wa kazi zinazoanza saa 12 jioni hadi 12 asubuhi, mwanga ukiwa ni uleule tofauti na awali taa ziliwaka kwa saa sita, baada ya hapo mwanga unapungua na kuwa hafifu, hata wanashindwa kufanya kazi .

“ Kwa sasa tunauhakika wa kazi kwa usiku mzima tunafanya kazi sawa na asilimia 95 tunaweza kupata debe za dagaa kuanzia 60 mpaka 70 tofauti na awali tulikuwa tunapata 30 hadi 40 na kutokuwa na hofu ya kulipukiwa na petroli sasa ni mwendo wa kazi tu..” anaeleza Faustine.



Wavuvi wakiweka taa zinazotumia nishati ya jua kwenye mitumbwi yao kwa ajili ya kwenda kuvua dagaa, **PICHA: NEEMA EMMANUEL.**

**MKAUSHA SAMAKI**

Anna Said, mkaushaji dagaa katika mwalo huo, anaeleza awali biashara yao ilikuwa ni tatizo, wakianika chini mvua ikinyesha zinasombwa na maji na ikinyesha kwa siku mbili dagaa zikipata maji mzigo wa shilingi millioni moja, wanachokiambulia ni laki mbili, laki nane ‘inakata’, hivyo matarajio yao mradi mpya ni ukombozi katika biashara zao.

Anasema mvua ni hatari kwa dagaa wanaponyeshewa, wanaoza ikizingatiwa maeneo yao walikuwa wakitumia kuanika kwenye vichanja visivyo na ‘vikingio’. Mradi ulipobisha hodi katika eneo lao, anasema hawakusita kutoa eneo, kwani waliona ni nuru iliyowatembelea.

“ Dagaa zinazokaushwa hapa ni bora sana tofauti na tulizokuwa tunaanika awali tunaiomba serikalimradi huu uwe endelevu na usije ukaishia njiani ili uweze kutuokoa na kutuinua kiuchumi kwa sababu hapa dagaa zinakaushwa kwa muda mfupi, tena sio kwa uwazi.

“Hata kama mvua ikinyesha zipo salama, zinaoshwa vizuri na wanaweka chumvi na kuzifanya zikae kwa muda mrefu tofauti na zile zetu za awali, “ anaeleza said.

Aidha, Johness Mashange ni Mwenyekiti wa Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi ndani ya mita 60 kutoka mwambao mwa ziwa (BMU) na msemaji wa wavuvi Kanda ya Ziwa, anaeleza kuwa teknolojia hiyo inaleta mabadiliko na tija kiuvuvi kwa sababu mwaga wake umefanyiwa utafiti mavuno uzalishaji unaongezeka kwa wingi hivyo wanaendelea kuwahamasisha wavuvi watumie njia hiyo bora kwa manufaa yao na kukuza uchumi wa nchi.

**BOSI KIWANDANI**

Diana Mbogo ni Mkurugenzi Mkuu wa kiwanda cha ukaushaji na uchakataji dagaa, Millennium Engineers anaeleza kuwa mradi wa kukausha dagaa kwa kutumia mtambo wa umeme jua pamoja na usambazaji wa taa za kuvulia dagaa zinazotumia nishati ya jua unaenda kukidhi na kusaidia shughuli za uvuvi katika eneo Hilo katika uzalishaji na ukaushaji na kuondokana na adha ya majanga ya moto wanapokuwa ziwani.

Anaeleza kuwa kampuni hiyo kwa ufadhili wa serikali kupita Wakala wa Nishati Vijijini ( REA ), wamewaletea taa hizo na mitambo ya kisasa ambayo ni ya kwanza Afrika Mashariki inayosaidia kukausha dagaa tani 1.2 kwa muda mfupi na kuzifanya kuwa na ubora unaokidhi viwango vya kimataifa.

Lengo analitaja ni kuondokana na matumizi ya karabai ambayo inatajwa kuleta madhara mbalimbali ikiwemo mlipuko na kuhatarisha maisha ya wavuvi na viumbe vinavyoishi majini pia wavuvi hao, pia wamekuwa wakitumia taa za vibatari na tochi za betrii ambazo zimekuwa hazikidhi mahitaji yao zikiwa na mwanga mdogo na kuzimika kabla ya kazi kumalizika .

Anaeleza kuwa wavuvi hao kwa siku wanakodishwa kwa bei nafuu 2500 sawa na bei walioyokuwa wakitumia kukodisha ama kuchaji betri zao pia kiwango hicho ni chini asilimia 30 ukilinganisha na wale wanaotumia karabai pia wanauwezo wa kuzinunua na kuimiliki mwenyewe kwa kulipia kidogokidoga sh. 350000 kwa miezi mitatu.

“Mpaka sasa taa zilizopo ni 500 wanategemea mradi mzima kuwa na taa 1000 ambazo zitawasaidia wavuvi 225 pia gharama za ukaushaji ni 300 kwa kila kilo mitambo hii inatumia mionzi ya jua inasaidia sana upotevu wa chakula unaosababishwa na kuoza kwa dagaa hasa vipindi vya mvua, ,dagaa kutokuwa na ubora kwa sababu uchakataji unaotumika ni kuwamwaga chini kwenye sakafu au kuzianika kwenye vichanja juu zikiwa wazi hapa utakausha tani 1.2 kwa masaa matatu hadi manne,” anaeleza Mbogo

Mkurugenzi wa Teknolojia za Nishati Jadidifu na Mbadala kutoka REA Mhandisi Advera Mwijage, anaeleza kuwa jukumu lao kubwa ni kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ,salama maeneo ya vijijini hivyo serikali imefadhili million 560 katika mradi huo ambazo ni asilimia 30 ya mradi wa zaidi ya Sh.Billion 1.5 pia unatumia nishati inayolinda mazingira.

Anaisema lengo ni kuhakikisha miradi ya nishati vijijini inakuwa na matumizi ya kiuchumi na kuzalisha fursa mbalimbali na kuhakikisha wananchi wanapata huduma kwa bei wanayoweza kuimudu na isiyokuwa na makali hivyo kupitia fedha za serikali zitanunuliwa taa 536 na mitambo mitatu ya kukaushia dagaa.

“ Walikuwa wanatumia vibatari ambavyo vikalishio vilitengenezwa na miti ukienda kwenye visiwa vyetu na maeneo ya pembezoni asilimia kubwa ya miti imekatwa kwa ajili ya matumizi ya karabai pia mafuta ya taa waliyokuwa wanabeba kwenda nayo ziwani wakati wanaweka mafuta kwenye taa yanamwagikia ziwani na kuwa tatizo kwa viumbe vilivyopo majini ,” anaeleza.

**MMILIKI MTUMBWI**

Victoria Japhet, mmiliki wa Mtubwi wenye jina la Mv. Mama anaeleza kuwa yeye ametoa ajira kwa vijana wanne na biashara hiyo inalipa hasa kipindi hiki wanapotumia nishati hiyo kuvulia dagaa kwa sababu taa za awali zilikuwa hazichukui muda na walikuwa wanatumia gharama za mara kwa mara kununua tofauti na hizo zinakaa muda mrefu ata zikiharibika wanazirejea na kupewa fedha kwa ajili ya ahsante hivyo wavuvi hawazitupi tena ziwani awali zikiharibika wanazitupa hukohuko.

“Taa za betri mara nyingi zikiwazimikia au kuharibika wanazitupa majini inakaa miaka inaanza kuvuja taratibu inachangia uharibifu wa mazingira hizi za sasa hawawezi kuzitupa kwa sababu ukirudisha unapewa ahsante napenda kutoa wito hasa kwa akina mama waingie kwenye hii biashara ukweli inalipa wasiogope,”anaeleza

Aidha, Mhandisi wa mradi huo Wistone Nnko, anaeleza kuwa dagaa wanakaushwa kwa masaa matatu hadi manne wanatoka wakiwa bora wenye thamani na anaoweza kukaa kwa muda mrefu bila kuharibika kwani wanaokaushwa kwenye vichanja siyo salama kwa sababu ndege wanatua kwenye dagaa hizo vumbi lenye mchanga

“Ukweli dagaa za kukaushiwa chini na kwenye vichanja mazingira hayo siyo rafiki lakini hizi mazingira ni safi hakuna ndege anayeweza kuingia wala hewa yenye mchanga inayo itapita”anaeleza

Meneja Uendeshaji wa Millennium Engineers Enterprises David Mbaga anaeleza kuwa dagaa wanapofikishwa kiwandani hapo wanaoshwa kwa ubora kwa kutumia maji ya chumvi zinachakatwa baada ya hapo zinapelekwa kwenye kaushio kwa ajili ya kukaushwa

# TUNAVYOTUNZA MAZINGIRA KWA UCHUMI ENDELEVU, HADI LENGO 2025

**Na Flavian Jeremiah**

JAMANI, mazingira ni vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu, kwa mfano miti,maziwa, mito na hewa.

Mazingira na binadamu ni vitu viwili vinavyotegemeana, hivyo kuna wajibu wa kuhakikisha yanatunzwa kwa lengo la ‘kusapoti’ maisha ya binadamu na usalama wa viumbe hai vingine.

Idadi kubwa ya watu wana uelewa kuhusu mazingira, changamoto ni jinsi gani ya kuyatunza mazingira, pamoja na kufanya shughuli zetu pasipo kuwa na uharabifu mkubwa kwenye mazingira katika kuendeleza uchumi wa mtu mmoja mmoja mmoja, na taifa.

Hivyo ni hali inayofungua wajibu wa wote kuyatunza mazingira na halibaki kwa mtu mmoja au chombo fulani cha serikali na taasisi binafsi tu.

Serikali imeweka vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2023/24 kama miradi ya kitaifa kupunguza uharibifu wa mazingira, pamoja na programu mbalimbali ikiwemo upandaji mti kwa ajili ya kupunguza athari za mazingira na mabadilko ya tabianchi.

Jamii inaweza kupanda miti, ufugaji na uvunaji wa kisasa wa nyuki pasipo kutumia moto kulinda misitu na kupata kipato kikubwa,matumizi ya taka ngumu kutengeneza mkaa “bio

briquette” badala ya kuchoma miti kutengeneza mkaa, uyoga, vyakula vya ndege wa kufugwa kama kuku na bata.

Kutokana na takwimu za Benki ya Dunia ya mwaka 2019, asilimia 70% ya Watanzania wanaishi vijijini na wanategemea maliasili ‘kusapoti’ maisha yao.

Changamoto kubwa kwao ni uelewa mdogo wa njia bora za matumizi ya maliasili hayo kwani idadi kubwa wanaangalia wakati wao pasipo kufikiria kizazi kijacho.

Utupaji wa taka sehemu zisizo sahihi ni jambo ambalo limekuwa likiendelea kuathiri ubora na wingi wa maji kwenye vyanzo vya maji nchini hivyo kupelekea upungufu wa maji kwenye baadhi ya mikoa mfano Dar es Saalam, hata inachangia ongezeko la magonjwa ya kansa yanayochangiwa na utiririshaji maji machafu yenye mchanganyiko wa kompoundi mbalimbali zenye hyrdokaboni.

Pia, kuna athari kwenye maisha ya viumbe wanaoishi majini kisha kurudi kwenye mzunguko wa chakula(food chain) kutoka kwa wanyama au samaki kwenda kwa binadamu inayofanya athari za kiafya na kuathiri uchumi. Asilimia 88 ya Watanzania bado hutegemea kuni na mkaa kama sehemu kubwa ya nishati yao ambayo imepelekea janga kubwa la upotevu wa miti (misitu), mabadiliko ya tabianchi, kupungua kwa rutuba za udongo.

Inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2050 watu wanaoishi vijijini wanategemea kuongezeka kufikia asilimia 80, hivyo kila mmoja ana wajibu wa kuhakikisha anayatunza mazingira kwa kufanya shughuli zake pasipo kuathiri mazingira.

Mfano upo kwenye kuepuka matumizi ya sumu na vifaa visivyo kubaliwa kuvulia samaki,na kuepuka ukataji holela wa miti na uchomaji wa misitu,ufugaji na uvunaji wa kisasa wa nyuki.

Ombi letu kwa serikali ni kutengeneza sera endelevu za utunzaji wa Mazingira pamoja na vyombo vyake (NEMC) kusimamia kwa uadilifu projekiti zote kubwa kufanyiwa tathimi ya athari ya


mazingira pamoja na kuhakikisha matibabu ya taka hatari (maji,taka ngumu) taka hatari kutoka viwandani, migodini n.k ,yanakidhi ubora unaotakiwa kuendenana na sheria ya usimamaizi wa mazigira ya mwaka 2004.

Wakala wa misitu Tanzania (TFS) kwa kushirikiana na wizara ya maliasili ya utalii pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, iendelea kutoa programu mbalimbali za mazingira, kama vile elimu, uhamasishaji kupanda miti na kuwapatia miti wananchi ambazo zinaweza kupunguza athari za mazingira.

Pia, kuna kuendelea kuandaa mikakati ya kupunguza matumizi ya mkaa na kuni kama uhamasishaji wa matumizi ya mkaa mbadala “bio briquettes”, umeme na gesi asilia vyanzo vingine vinavyo endana na uhalisia ya uchumi ya idadi kubwa ya Watanzania (nafuu na nishati safi) ili kuendana na lengo la 7 ya maendeleo endelevu( SDGs 7) na kufanikisha hatima ya serikali kusitisha matumizi ya kuni na mkaa 2024-2025.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Jamani tujipange, kipindupindu kimeua Kagera, nasi tukae mkao wa tahadhari






NA SABATO KASIKA

KIPINDUPINDU kinatajwa na wataalam wa afya kuwa ni ugonjwa wa kuambukiza ambao husababisha kuhara kwa maji mengi, na kuchangia upungufu wa maji mwilini na wakati mwingine mauti.

Mauti hayo huchangiwa na kutotibiwa, kwa kuwa mara nyingi bakteria ya kipindupindu hupatikana katika maji au vyakula vilivyochafuliwa na kinyesi kutoka kwa watu walioambukizwa vijidudu vya kipundupindu.

Ugonjwa huo huathiri zaidi na kusambaa katika maeneo yenye huduma duni ya maji, usafi wa mazingira, na kwamba bakteria wa kipindupindu wanaweza pia kupatikana katika mito.

Hapa nchini, baadhi ya maeneo huwa yanakumbwa na ugonjwa huo mara kwa mara na kusababisha vifo, huku jamii ikiaswa kuzingatia usafi kuanzia kwenye utunzaji wa chakula, maji ya kunywa na hata vyoo.

Dar es Salaam ni miongoni mwa maeneo ambayo huwa yanakumbwa ugonjwa huo hatari, lakini angalau kwa muda mrefu kidogo kumekuwa na unafuu kwani matukio ya kipindupindu sio mengi kama zamani.

Wakati Dar es Salaam kunaendelea kuwa kimya bila kuripotiwa kuwapo kwa ugonjwa huo, mkoa wa Kagera unatajwa kuvamiwa na kipindupindu ambacho kimesababisha vifo vya watu wanne.

Hivyo, ninadhani ni vyema iwapo mikoa mingine ikachukua hatua za kujilinda dhidi ya ugonjwa huo, kwa kuzingati usemi wa kiswahili kuwa ‘ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia zako maji’.

Ni muhimu Watanzania kukumbuka kuwa bakteria wa kipindupindu ndio chanzo kikuu cha ugonjwa huo, ambao huenezwa zaidi kupitia chakula na maji yaliyochafuliwa.

Kwa mujibu wa wataalam wa afya, bakteria hao wanapoingia ndani ya mwili wa mwanadamu, hutoa sumu mbaya kwenye utumbo mdogo, na kwamba sumu hiyo baadaye husababisha upotezaji wa maji zaidi.

Hivyo, kinachotakiwa ni usafi, hasa kuandalia vyakula katika mazingira safi, kunawa maji na sabuni baada ya kutoka msalani, kuchemsha maji ya kunywa na pia kuosha matunda na maji ya uvuguvugu.

Bahati mbaya baadhi ya watu huwa hawazingatii maelekezo hayo na kujikuta wakihatarisha afya zao pasipo kujua au wakiwa na wanajua kitakachowapata baada ya kufanya makosa.

Ninadhani ni vyema kubadili mfumo wa maisha, kuanzia nyumbani na hata mitaani kwa mama lishe wamekuwa wakipika vyakula, wengine wakiwa katika mazingira yanayohatarisha afya zao na za wateja wao.

Kwa mfano, baadhi hupika vyakula huku kukiwa na taka zilizojaa nzi ambazo wao huzizalisha, na wakati mwingine nzi hao husambaa hadi kwenye vyakula, kitendo ambacho kinaweza kusababisha magonjwa ya kuhara kikiwapo kipindupindu.

Kimsingi, usafi katika mazingira ya kuandalia chakula, msalani na ulaji wa matunda na vyakula vingine ni wa muhimu kwa ajili ya kuepuka ugonjwa huo unaopotea na kurudi.

Unarudi kwa sababu ya kuwapo kwa mazingira ambayo ni rafiki kwa ugonjwa wenyewe, hivyo kila mmoja hana budi kwa nafasi yake kuchukua hatua zitakazomsaidia kuuepuka.

Kugundulika kwa ugonjwa huo katika wilaya ya Misenye mkoani Kagera, kuwafanye Watanzania wa maeneo mengine kuchukua hatua za kujilinda dhidi ya kipindupindu ambazo ni kuzingatia kanuni za afya.

Mkuu wa mkoa wa Kagera Fatuma Mwassa anawakumbusha wakazi wa mkoa huo kuchukua tahadhari kwa kuepuka safari zisizo za lazima kwa kuwa ugonjwa huo ni hatari na unaambukiza kwa haraka.

Kwa kuwa Kagera ni sehemu ya Tanzania, inawezekana mkazi wa huo, mwenye dalili za kipindipundu akasafiri hadi Dar es Salaam au maeneo mengine ya nchi na kueneza ugonjwa huo.

Hivyo, kuna haja ya kuchukua tahadhari pia kwa lengo la kusaidia kuepuka ugonjwa huo ambao chanzo chake ni kutozingatia usafi wa maandalizi ya vyakula, maji na huduma nyingine muhimu kama choo.

UCHUMI

## MAZITO SEMINA ZA TGNP INAYOYAIBUA…

# Unyama jinsia mitaani unavyozaa shida afya, umasikini na kasoro kupata sheria

## •Mzizi wa harakati zao;Dk. Migiro, Lissu, Mnyika



Wanaharakati wa TGNP walipokuwa kwenye maadhimisho yao. **PICHA: PILLY KIGOME.**

**Na Pilly Kigome**

ILIKUWA Jumatano ya Oktoba 18 mwaka huu kuanzia majira ya saa nne asubuhi, wadau wa Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS) walikutana katika viwanja vya TGNP, Dar es Salaam kwa tarumbeta, huku wakifagia uwanja kwa nderemo na vifijo kwa nyimbo za kuzisifu semina elekezi za jinsia na maendeleo, zimewatoa walipo hadi sasa.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ukiadhimisha Tamasha la 15 la Jinsia, ikiandaa simulizi maalumu kutoka kwa washiriki wanaohudhuria Semina za Jinsia na Maendeleo, hadithi za mafanikio yaliyotokana na GDSS toka kuanzishwa kwake.

Zilikuwa simulizi na hadithi za zinayofurahisha na kusikitisha, mikasa na simulizi kutoka kwa wanasemina hao wa zamani na wapya.

**KUTOKA KWA WAKONGWE**

Anayeanzisha ni mama wa makamo, Subira Kibiga, mkongwe na mwanzilishi wa GDSS, anayetoa ushuhuda, mwanzo wa harakati za jinsia mwaka 1998, wakiwa watu watatu, mtandao ukiwa na makao yake makuu, Kariakoo kabla ya kuhamia Mabibo, Dar es Salaam, inakodumu hadi sasa.

Kibiga anasimulia, namna harakati zilikuwa ngumu wakati huo, maana elimu na shule kwake ilikuwa changamoto akilinganisha na wenzake walioenda darasani.

Anafafanua, walifanya harakati kwa shida na dhiki wakitembea kwa miguu, kupata semina elekezi. Kipindi hicho ilikuwa na mawasiliano ya tabu, wakati wanafanya hayo.

Hapo anaorodhesha changamoto za kukosa mawasiliano, hata wakapotezana na wenzake kwa muda mfupi, hata alipoenda ilikokuwa TGNP Kariakoo akaambiwa imehamia Mabibo, akapatafuta na hatimaye akafanikiwa, kuendeleza harakati ambazo hajaziacha hadi sasa.

Anasimulia haikuwa rahisi kusimama kupigania harakati hizo, kwa watoto wa siku hizo akisema hawawezi. Hapo akawa na mfano, binafsi alikuwa anatoka Kigamboni hadi Mabibo kwa shida, jambo analolitaja gumu kwa asiye mwana - harakati.

Subira anaeleza walipohamia Mabibo, TGNP wakaanza vikao na semina hizo chini ya mwembe na sasa upo kwenye majengo.

"Kwa kweli, mimi GDSS imenitoa mbali sana. Sasa najiamini, najua kupigania haki zangu, haki za wanawake wenzangu, napita kifua mbele kokote, lakini GDSS ndio iliyonijenga hadi kufika hapa nilipo," anasema.

Ni hoja inayoungwa mkono na Agness Lukanga, mkongwe wa GDSS, akisema amejiunga mwaka 1996, kipindi TGNP ikiwa na ofisi Posta, Dar es Salaam, yeye akiwa mwanafunzi mwaka wa kwanza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, akichukua masomo ya sanaa.

Anasimulia ilipofika mwaka 2006, alianza rasmi harakati zilizohamia chini ya mwembe, Mabibo akajifunza mambo mbalimbali ya ukatili kijinsia, yeye akishiriki kama msanii wa wa kikundi kilichojulikana kama 'binti leo'.

Kwa mujibu wa Agness, ni semina zenye maudhui yaliyofanyiwa utafiti, wakishirikisha jamii kupata mrejesho kwa ngazi za kata, wilaya na taifa.

Hapo anawaorodhesha wanaharakati wengi aliowataja kwa majina; Dk. Asha Rose - Migiro, Tundu Lissu na John Mnyika, ambao baadaye wakawa wanasiasa maarufu.

**WADAU WAANDAMIZI**

Abbas Mzelu, anataja kuifahamu GDSS mwaka 2019, akinena kwamba semina zimemjenga na kumpa ujasiri wa kujua changamoto za kijamii, hata kujitambua katika haki zake, kufahamu sheria na hadi sasa analea mabinti katika harakati hizo akiwajengea uwezo.

Mzelu anakiri kuwapo manufaa mengi, ya watu kujitambua na semina inawapatia ujasiri kujisaidia wao na jamii inayowazunguka kwa changamoto mbalimbali.

Tabu Ali, kutoka Kituo cha Maarifa na Taarifa (KC) ya Majohe, ana ushuhuda kuwa GDSS imemsaidia na jamii yake, amekuwa jasiri kuibua changamoto za wanawake wanaokabiliwa na shida.

Anaeleza ameshaibua changamoto nyingi za wanawake wenzake, akiwamo (jina tunalo) mzazi wa watoto watano aliyefanyiwa ukatili na aliyekuwa mumewe, baada ya mume kuzaa na mtoto wake wa kwanza na kumbaka binti yake wa pili bila yeye kufahamu, wakati hayupo nyumbani.

Tabu anasimulia mkasa ulianza mwezi Juni mwaka huu, akipigiwa hodi na wanywaji pombe za kienyeji waliotoka kwenye moja ya vilabu jirani na anapoishi, wa eneo la Majohe, wilayani Ilala alikoishi wakamletea habari kuna mwanamke hana pa kwenda, analala kilabuni.

Anasimulia aliwachukua wenzake kuelekea kilabuni, wakamkuta mama huyo na watoto wake katika mazingira magumu yasiyo rafiki kimaisha.

Baada ya kumhoji, wakapata ufafanuzi kwamba alikuwa Chalinze, mkoani Pwani katika kijiji cha Pingo na mumewe (jina tunalo) wa umri miaka 44, walipooana mwaka 2014, yeye akiwa na watoto wawili wa kike.

Kipindi anaolewa, anasema binti mmoja alikuwa na miaka miwili na mdogo miezi nane, wakaanza maisha na akabahatika kuongeza watoto watatu na mume huyo, wakijishughulisha na kilimo.

Anasimulia, kufika mwezi Juni mwaka huu, mama huyo alienda Dar es Salaam kumuuguza baba yake, akiwaacha wanawe nyumbani kwa kuwa walikuwa wanasoma.

Pi, anasema, wakati anamuuguza baba yake, mume wake nyuma alimbaka binti yake mkubwa, huku akimpa vitisho ikiendana na kupata ujauzito, binti akiwa darasa la sita.

Mama huyo aliporudi nyumbani, anasema akahisi binti yake yuko katika mabadiliko makubwa na akamchunguza kugundua ujauzito. Hakunena naye kwa kina akimsubiri ajifungue na baada ya hatua hiyo, binti akajibu mimba hiyo ni ya baba yake mlezi, alibakwa.

Wakati kuna mkasa huo, mama huyo anasimulia wakati mwingine alipotoka, baba huyo akambaka binti mwingine, kipindi hicho alikuwa darasa la nne, naye mtoto akakiri kabakwa na mzazi.

Anasimulia, kwa msaada wa majirani na viongozi mtaani, walilifikisha polisi, lakini baba huyo akaachiwa huru, licha ya kipimo cha daktari kuthibitisha kuingiliwa kwa mtoto huyo.

Mwana GDSS huyo anasema, kwa sasa wanashughulika na mwanamke kusimamia haki zake kwanza kisheria, pia suala la binti na wanafunzi kuzalishwa kwa kubakwa.

Tabu kupitia semina hizo, akaibua changamoto nyingine, mwanamke (jina tunalo), mkazi wa Gongolamboto, Dar es Salaam, aliyepata ulemavu wa masikio kwa kipigo cha mumewe, ambaye akataka kupokonywa haki zake walizochuma wawili.

Baadhi ya mateso ya mwanamke huyo anasimulia, mume akajenga tabia anapotaka kujisaidia haja ndogo anamwagia mkewe, mithili ya mboga bustanini.

Ni magumu kuamini ambayo yakaunganishwa na mkasa aliouibua mtoto (jina tunalo) anayesoma shule wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani aliyekuwa akiingiliwa na baba yake mzazi, mara baada ya mama yake kuachana na baba huyo.

Hiyo ni pale binti aliyebakishwa kwa baba, akiwa darasa la kwanza kipindi hicho. Simulizi inadai mtoto huyo kwa sasa anasoma darasa la nne, kijamii anakosa raha akitaniwa na wenzake hata anaathirika kisaikolojia, huku afya yake ikiwa dhaifu.

Ni simulizi ya kina namna, mtuhumiwa alifikishwa mahakamani Bagamoyo, akaachiwa huru katika mazingira tata, licha ya kuwapo marejeo ya uthibitisho wa vitendo madaktari. Inadaiwa kwa sasa mtoto huyo hana uwezo haja ndogo kwa kipindi kirefu.

"Sisi tunashangaa ndugu mwandishi yaani baba wa mtoto huyu yuko nje na anajinadi kuwa hakuna anayemuweza kwani yeye mshirikina na hakuna atakayemfunga kwani mtoto wake mwenyewe" anafafanua, Amina msimamizi wa mtoto huyo, huko Bagamoyo.





# Wanaotetea haki watoto, jinsia watakiwa kwenda pembezoni

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, ameagiza mashirika yanayotekeleza miradi ya haki za kijinsia na watoto kujikita katika maeneo ya pembezoni kwa sababu ndiko kwenye matatizo.

Dk. Chana alitoa kauli hiyo juzi wakati wa hotuba yake ya ufunguzi wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kwa mkoa wa Dodoma.

Aliyataka mashirika hayo yanayojihusisha na kutetea haki za kijinsia na watoto kujikita maeneo ya pembezoni hasa vijijini kwa sababu ndiko kwenye shida kubwa.

Alibainisha kuwa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia bado haijafika na mashirika hayo wajikite ili kuwasaidia wananchi kunusurika na vitendo vya ukatili.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia vinafanyika katika maeneo hayo kutokana na kukosa elimu ya kujikinga na ukatili unaofanywa na watu baki pamoja na ndugu wa karibu wa familia hizo.

Kadhalika, alisema kumekuwapo na sababu nyingi zinazoelezwa ya ongezeko la ukatili wa kijinsia nchini na ikiwamo hali ngumu ya maisha ambayo huleta msongo wa mawazo na kujikuta wakitenda matukio.

Alisema sababu nyingine ni mila na tamaduni kandamizi pamoja na kushamiri kwa mfumo dume katika jamii.

Alitaja sababu zingine kuwa ni matumizi mabaya ya teknolojia ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababisha vijana kufanya vitendo vya kikatili hasa ubakaji wa watoto na wanawake pia kulawiti.

Kadhalika, mmomonyoko wa maadili katika jamii unaochangia vitendo hivyo kushamiri kila siku licha ya kuwapo kwa sheria kali inayokataza matukio hayo.

Alisema waathirika wakuu wa matukio ya ukatili wa kijinsia ni wanawake na watoto ingawa takwimu za wanaume wapo, lakini ni wachache kulinganisha na kundi lingine.

Alisema serikali imeanzisha madawati ya ulinzi na usalama katika shule za msingi, sekondari na taasisi za elimu ya juu na kati ili kuhakikisha kuwa elimu kuhusu madhara ya ukatili inatolewa na vijana wanajengewa uwezo wa kutoa taarifa na kupatiwa msaada wa kisaikolojia.

Alisema hadi sasa madawati 1,850 yameanzishwa kati ya hayo 772 ni shule za msingi na sekondari kwa upande wa taasisi za elimu ya juu lengo ilikuwa kuanzisha madawati 612 ifikapo Juni 2024 hadi sasa yaliyopo ni 273.

Meneja Mipango wa Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Katharina Kuehn, alisema wanashirikiana na serikali kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia.

Kuehn, alisema katika siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia GIZ imetoa elimu kwa wanafunzi wa Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM) kusaidia na kuzuia vitendo vya ukatili.

Baada ya uzinduzi huo watashirikiana na UDOM kwenda baadhi ya maeneo ya vijiji vya Wilaya ya Bahi mkoani hapa kutoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia kwa wananchi.



Wafanyakazi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, kitengo cha usafi wa mazingira wakiondoa takataka zilizorundikana kwenye soko la Sabasaba jijini humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watendaji watakiwa kusimamia sekta kilimo kwa maendeleo

**Na Elisante John,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka watendaji wa kata na vijiji, kusimamia sekta ya kilimo ili wakulima hasa vijana waongeze uzalishaji wa alizeti, kutoka asilimia 50 msimu uliopita na kufikia asilimia 70, msimu huu.

Serukamba, alisema hayo juzi alipokutana na watendaji wa kata, vijiji na maofisa ugani, katika kikao cha pamoja, kilichofanyika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba kwa lengo la kuongeza maeneo ya kilimo kwa ajili ya msimu huu.

"Hapa sitanii nataka kila mmoja ajiandae kusimamia suala hili, vijana kwenda shambani ni suala la lazima, tukifanya hivyo tutaongeza mavuno na tutawaondolea watu wetu changamoto ya umasikini.

"Nataka kuona mkoa wa Singida unaingia kwenye historia ya kuzalisha mafuta ya kula hapa nchini," alisisitiza Serukamba.

Alisema msimu uliopita alizeti iliyozalishwa nchini, Mkoa wa Singida ulichangia asilimia 50, lakini msimu huu anataka Singida ifikishe asilimia 70 na kiwango hicho kitafikiwa iwapo wakulima wataongeza nguvu zaidi kwa kushirikiana na wataalamu wa ugani, watendaji wa vijiji na kata.

Kuhusu upatikanaji wa mbegu bora, Serukamba alisema serikali imekubali kuupatia Mkoa wa Singida mbegu mpya aina ya Haysan, ambayo itauzwa kwa bei ya ruzuku, lakini kwa fedha taslimu na kutoa nafuu kwa mkulima kuzalisha zaidi alizeti.

Pia, alisema inapatikana kwa wingi na mkulima anapaswa kuonana na ofisa ugani wa eneo lake ili apatiwe kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao, ikiwamo zao la alizeti.

"Kilimo chetu hakiwezi kuwa cha tija kama hatutatumia mbolea, naomba sana tuwasimamie watu wetu watumie mbolea, tukifanya hivi halmashauri nayo itanufaika kwa kupata mapato yatakayotekeleza miradi na shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema.

Wakizungumzia mkakati huo, baadhi ya watendaji akiwamo, Gelege Kingu, wa Kata ya Kiomboi, aliahidi kwenda kusimamia wakulima ili waongeze uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, katika maeneo yao.

"Haya maelekezo tuliyopata leo, naamini yatakuwa chachu katika kuhakikisha tunawahamasisha wakulima wetu kuongeza umakini...

"Vijana ni nguvu kazi kubwa na ni kundi muhimu katika kuhakikisha kilimo kinafanikiwa na kupiga hatua kubwa, iwapo kila mmoja wao atafuata kanuni bora za kilimo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alimhakikishia Mkuu wa mkoa kuwa maeneo yaliyoainishwa kupitia kikao hicho, atahakikisha yote yatalimwa, kutunzwa na wakulima watatumia mbegu bora na mbolea, ili kuongeza uzalishaji wa mazao.

Kupitia kikao hicho, kwa pamoja walikubaliana kuwa halmashauri ya Wilaya ya Iramba, itaongeza eneo la kilimo linalofikia ekari 3,464, katika msimu huu wa kilimo 2023/2024, kwa ajili ya mazao mbalimbali, yakiwamo ya chakula na biashara.

# 'Serikali ifanyie kazi upungufu ushiriki wanawake wenye ulemavu kugombea uongozi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHUO cha Serikali za Mitaa Hombolo (LGTI), kupitia wanazuoni na wanataaluma wake wameishauri serikali kufanyia kazi upungufu ikiwamo ushiriki mdogo wa wanawake na watu wenye ulemavu katika kugombea nafasi za uongozi ili kupata viongozi bora kwa maslahi ya taifa.

Naibu Mkuu wa Chuo hicho Taaluma,Utafiti na Ushauri wa Chuo Dk. Michael Msendekwa alitoa ushauri huo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye kongamano la 15 la wanazuoni.

"Leo tumekuwa na kongamano la 15 la wanazuoni ambapo pamoja na kuongelea mambo mengi, lakini kubwa ni kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa wa 2024 kama kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii nchini.

"Tumekuja na mada hii kutokana utafiti uliofanywa na wanazuoni kuonesha wanawake hawashiriki katika uchaguzi kama wachaguliwa bali wanachagua hivyo tumejadili ni jinsi gani wanawake wanaweza wakashiriki katika uchaguzi huo kwasababu imeonekana kuwa ushiriki wao ni mdogo hususani kwenye kupigiwa kura," alisema Dk. Msendekwa.

Pia, walijadili jinsi watu au uchaguzi wa viongozi unaweza ukachochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Alisema wanazuoni wameona kuwa wakichaguliwa viongozi wazuri katika mamlaka za serikali za mtaa watakuwa ni kichocheo kizuri katika kuleta maendeleo kiuchumi na kijamii.

"Maana yake hawatataka rushwa wala kitu chochote kwasababu tayari wao wenyewe wameendelea kiuchumi na kijamii kwahiyo hizi mada zitatusaidia sana katika kuboresha au kama kichocheo kikubwa katika uchaguzi wetu wa serikali za mitaa 2024.

"Tunashukuru na kuishauri serikali ichukue haya maoni yetu mapendekezo ya wanazuoni ambayo wameyajadili ili wayafanyie kazi kwasababu maoni na mapendekezo haya yamejikita sana katika utafiti kwahiyo mambo ambayo yalikuwa yanaongelewa tumefanya utafiti katika mambo mengi ya maendeleo," alisema Dk. Msendekwa.

Kadhalika, alisema wanataka uamuzi wa serikali uwe unatokana na utafiti ambao hutoa majibu au taarifa ya vitu vinavyotakiwa kufanywa na ni mada ambazo zimetokana na utafiti mbalimbali.

"Kwahiyo tutazitengeneza na kuzipeleka serikalini na kushauri kuwa haya mapendekezo yanatokana na utafiti mbalimbali na yakizingatiwa hayo tutaboresha uchaguzi wetu na uchaguzi wetu tatapata maendeleo ambayo tunakusudia maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa nchini," alisema Dk. Msendekwa.

Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Mashala Lameck, alisema kongamano hilo la wanataaluma ambalo linafanyika siku moja kabla ya mahafali kwa kila mwaka wamechagua mada ya uchaguzi wa serikali za mtaa na kuwa wanaangalia mchango wake katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa Watanzania.

"Mada hii ni nzuri kwa maana inatupa muelekeo tunavyoelekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwakani, utupe sasa mawazo kupitia wanataaluma ambayo yataisaidia sasa serikali katika kuboresha uchaguzi huo kwahiyo kongamano la leo lina akisi kabisa tukio la mwakani la kupata viongozi katika ngazi za msingi za mamlaka za serikali za mitaa.

"Kwahiyo itachangia katika kushuari sisi kama watafiti wana taaluma kuishauri serikali maboresho yatakayofanyika ili uchaguzi wa serikali za mitaa uwe na tija mwakani,





# Ukosefu elimu chanzo unyanyasaji mitandaoni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

IMEELEZWA kuwa licha ya kuwapo kwa sheria inayodhibiti maudhui mtandaoni, vitendo vya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia kupitia mitandao hiyo bado vinaendelea kukithiri kutokana na watumiaji wengi kutokuwa na uelewa kuhusu sheria hiyo.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, Dunstan Ndunguru, aliyasema hayo juzi jijini Mbeya wakati akifungua mafunzo ya Mahakama ya Mfano kwa wanafunzi wa vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Chama Cha Majaji na Mahakimu Wanawake Tanzania (TAWJA).

Mafunzo hayo yalitolewa kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Kampasi ya Mbeya na wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Mbeya (CUCoM) lengo la kuwajengea uwezo juu ya ukatili mtandaoni na namna ya kushughulikia mashauri ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto mitandaoni.

Alisema serikali ilifanya tathimini ya madhara yatokanayo na makosa mtandaoni ndio maana ikatunga sheria ya makosa mtandaoni ya mwaka 2015 inayotoa adhabu ikiwemo kifungo na faini.

Alisema kutokana na uelewa mdogo wa jamii na makosa hayo kutofikishwa mahakamani mara kwa mara watumiaji wengi wamepuuza sheria hiyo.

Aidha alisema unyanyasaji ni udhalilishaji unaoathiri jamii hasa vijana, wanawake na watoto hivyo ni muhimu kutoa elimu ya kupinga ukatili mitandaoni pamoja na kuelimisha jamii kujua haki zao wanapokutana na vitendo hivyo.

"Nimejulishwa kuwa kaulimbiu mwaka huu kwa upande wa mahakama ni kupinga ukatili mitandaoni, kauli mbiu hii ni muhimu katika kipindi hiki cha ukuaji wa teknolojia ambapo ukatili wa kijinsia mitandaoni umekithiri," alisema Jaji Ndunguru.

Alisema kaulimbiu hiyo itaongeza uelewa kwa jamii katika kuimarisha mifumo iliyopo na kukomesha ukatili wa kijinsia uliopo mitandaoni.

Aliongeza kuwa ili kuzuia ukatili na unyanyasaji mitandaoni lazima kuelewa na kuziheshimu mila za Kitanzania na kutambua kwa kuna madhara hivyo inampasa kila mtu kutumia teknolojia na mitandao ya kijamii kwa namna nzuri.

Aliwataka wanafunzi wa vyuo ambao wamekuwa miongoni mwa watumiaji wakubwa wa mitandao ya kijamii kutumia katika mawasiliano chanya na kuwa mabalozi wazuri wa kupinga ukatili wa mitandaoni na kutengeneza mazingira salama kwa kila mmoja. Makamu Mwenyekiti wa TAWJA, Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kanda ya Mbeya, Victoria Nongwa, alisema wametumia kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia mitandaoni ili kila mmoja ajilinde mwenyewe na wengine kwa kuzingatia sheria na maadili ya Mtanzania.

Alisema mafunzo hayo wataendelea kuyatoa kwa makundi mbalimbali ya kijamii ili kuhakikisha kunakuwepo uelewa wa pamoja kwa watanzania wakiwemo wasimamizi na watekelezaji wa sheria hizo.

## Mkurugenzi Ludewa akemea kilimo pembezoni mwa vyanzo vya maji

**Na Elizabeth John,** LUDEWA.

WANANCHI wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa mkoani Njombe, wametakiwa kuacha utamaduni wa kulima pembezoni mwa vyanzo vya maji maarufu kama vinyungu ili kuepuka uharibifu unaosababisha watu kukosa maji.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Mkurugenzi Mamlaka ya Maji Ludewa Mjini(LUDUWASA), Mhandisi Enock Ngoyinde alisema kilimo na ufugaji kwenye vyanzo vya maji limekuwa tatizo kubwa katika halmashauri hiyo.

"Kuna ambao wameshaingia hadi ndani kwenye vyanzo vya maji kwa kulima bustani za vitunguu,mahindi hata maharage eneo ambalo ni chanzo cha maji chenyewe, lakini pia kuna uchomaji wa moto hovyo kiasi kwamba maeneo yote ya vyanzo vya maji tayari yapo wazi," alisema Ngoyinde.

Alisema kuwa changamoto hizo zimesababisha hali kuwa mbaya ya upatikanaji wa maji na hivyo kuweka mkakati wa kuhakikisha wanafanya oparesheni kwenye vyanzo vyote vya maji.

"Baadhi ya wananchi tuliwakuta huko site tuliongea nao na kuwaelekeza waondoke mara moja maeneo hayo. Kwa mfano kuna chanzo kinajengwa mradi mpya, sasa eneo hilo wananchi walichodai waliona tumenyamaza kwa muda mrefu wakahisi tumeacha kwa hiyo wakawa wameingia," alisema Ngoyinde.

Hata hivyo, alisema vyanzo vya maji ambavyo vimeharibika kabisa ni vinne kati ya nane na hivyo kuendelea kuelimisha wananchi madhara ya uhalibifu katika vyanzo vya maji.

"Madhara ya uhalibifu wa vyanzo vya maji ni makubwa sana, sio ya mtu mmoja mmoja yanahatarisha uwepo wa huduma ya maji kote, sasa huduma ikishakua hafifu haikumbi mtu mmoja bali hata jamii ndio inaathirika," alisema Ngoyinde.

Ngoyinde pia alisema ili kukabiliana na changamoto hizo wanatumia mikutano ya serikali za vijiji ili kutoa elimu kwa wananchi waweze kutambua madhara ya kufanya uhalibifu kwenye vyanzo vya maji.




Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Damas Mapunda, akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo kwa kamati za maliasili na mazingira za vijiji vilivyopo katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu vinavyotekeleza Mradi wa SLR, jijini Mbeya juzi. Kulia ni Ofisa Kiungo wa mradi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Jacques Kempanju na Mshauri wa Kiufundi wa IUCN, Doyi Mazenzele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHUTCU yatoa msaada Kituo cha Afya cha Lupatingatinga

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA.

CHAMA Kikuu cha Ushirika wa Wakulima wa Tumbaku Wilaya ya Chunya katika Mkoa wa Mbeya (CHUTCU), kimetoa msaada wa vitanda vitatu kikiwemo cha kujifungulia katika Kituo cha Afya cha Lupatingatinga wilayani humo.

Aidha chama hicho pia kimekabidhi mashuka 20 katika kituo hicho kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wananchi wa kata hiyo pamoja na maeneo jirani.

Meneja wa CHUTCU, Christian Msigwa, alikabidhi misaada hiyo juzi kwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya,Mayeka Mayeka katika hafla iliyofanyika katika Kituo hicho cha afya.

"Mbali na vitanda na mashuka, pia tumeleta vifaa vya uchunguzi na taa maalum ambavyo vyote kwa pamoja vina thamani ya Sh 4,000,000, fedha hizi zinatokana na kilimo cha zao letu la tumbaku,"alisema Msigwa.

Msigwa alisema msaada huo ni takwa la kisheria kwa vyama vikuu na ushirika kuchangia huduma za kijamii na kwamba huo ni mwanzo wataendelea kugusa maeneo mengine yenye uhitaji.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Lupatingatinga, Dk. Obeid Prosper, alisema vitanda hivyo vitapunguza tatizo lililopo hasa kwa wajawazito wanapotaka kujifungua kwa kuwa kuna upungufu wa vifaa hivyo.

kituo hicho kinatakiwa kuwa na vitanda 10 vya kujifungulia lakini vilivyopo ni viwili pekee na hivyo akawaomba wadau wengine kuwasaidia ili kupunguza tatizo hilo.

Dk. Prosper alisema kwa wiki wanajitokeza wajawazito kati ya sita na saba wanaotaka kujifungua na hivyo idadi ya vitanda haiendani na idadi ya wanawake hao.

"Kuna wakati tunazidiwa na tunalazimika kutumia vitanda vya wagonjwa wa kawaida kwa ajili ya kujifungulia wajawazito,"alisema Dk. Prosper.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka aliushukuru uongozi wa CHUTCU kwa kujitoa kuchangia sekta ya afya na kwamba walichangia eneo muhimu kwa ustawi wa jamii.



## Serikali yaanza utekelezaji mitaala mipya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imeanza kutekeleza mageuzi yanayotokana na maboresho mapya ya sekta katika mitaala mipya ikiwamo shule za msingi na sekondari kuunganishwa na mawasiliano ya TEHAMA.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Ali Abdulgulam Hussein, alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akifafanua kuhusu matumizi ya mawasiliano ya TEHAMA kwa wanafunzi ambayo yatawawezesha kuingia katika mageuzi makubwa ya teknolojia hivi sasa.

Alisema ujenzi wa shule unaoendelea nchini katika hatua ya kwanza umezingatia upatikanaji wa vifaa vya maabara ambavyo vitawawezesha wanafunzi kuingia katika masomo ya sayansi na kupata ufaulu mzuri.

Alisema tayari Wizara ya Elimu imenunua vifaa vya maabara kwa shule zote za sekondari Unguja na Pemba ikiwa ni miongoni mwa vipaumbele vyake vya kwanza.

Aidha, alisema kipaumbele cha pili ni shule hizo kuunganishwa na mkongo wa taifa katika mawasiliano ya TEHAMA ambayo yatawawezesha wanafunzi kutumia vifaa vya kompyuta kwa ajili ya masomo yao.

"Mheshimiwa Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba ujenzi wa shule mpya za kisasa umezingatia upataikanaji wa vifaa vya maabara vya sayansi ambapo matarajio makubwa kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu," alisema.

Alisema katika ujenzi wa shule hizo masuala ya TEHAMA yamezingatiwa kwa kiwango kikubwa ili kuwawezesha wanafunzi kuingia katika ushindani wa sayansi na teknolojia.

Pia, kazi ya kusambaza huduma za TEHAMA kwa shule zilizopo mjini umefikiwa kwa asilimia kubwa na kwa sasa kazi ipo katika kufikisha huduma hizo vijijini pamoja na shule zilizopo katika visiwa vidogo vidogo Unguja na Pemba.

# Uvuvi haramu tishio uhai viumbe bahari, maliasili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi, wameitaka Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, kudhibiti matukio ya uvuvi haramu ambayo yanatishia uhai wa viumbe vya baharini na maliasili za matumbawe.

Akichangia muswada wa kuanzishwa kwa taasisi ya utafiti wa uvuvi wa maliasili za baharini katika kikao cha baraza la wawakilishi jana, mwakilishi wa jimbo la Kojani, Hassan Omar Hamad, alisema kumejitokeza kasi ya matukio ya uvuvi haramu unaotishia maisha ya viumbe vya baharini na mitego tishio kwa maisha ya samaki inatumika kwa sasa.

Aliitaka Wizara ya Uvuvi kupiga marufuku nyavu zenye macho madogo ambazo zinanasa samaki wadogo ambao hawafai kwa matumizi ya kula.

Aidha, alizitaja nyavu za kukokota baharini kuwa huharibu matumbawe ambayo ni mazalia ya samaki pamoja na aina mbalimbali za majani ambayo ndiyo chakula cha samaki.

"Wizara ya uvuvi na uchumi wa buluu tunawaomba waje na orodha ya aina zote za uvuvi ikiwamo zile ambazo hazifai kwa matumizi ya shughuli za baharini kwa sababu hivi sasa kumejitokeza uvuvi haramu unaotishia uhai wa viumbe vya baharini," alisema. Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani, Suleiman Makame Haji, alisema kuwapo kwa sheria ya utafiti wa uvuvi na maliasili za bahari ni muhimu ambao utawezesha kujua kiwango cha samaki kilichopo kwa ajili ya matumizi.

Alisema utafiti wa aina hiyo unahitajika na unakuja na jawabu sahihi kujua utajiri wa samaki waliopo pamoja na aina nyingine za samaki ambazo zipo katika tishio la kutoweka.

"Baadhi ya aina ya samaki ambao ni maarufu wameanza kupungua hatua kwa hatua na huu ni wakati mwafaka tuje na jawabu sahihi kujua sababu zake baada ya kufanya utafiti," alisema.

Aliwataja baadhi ya samaki ambao utafiti unahitajika ili kukabiliana na sababu za kupungua kwake ikiwamo pweza, ngisi na kamba ambao ni maarufu kwa soko la watalii ikiwa pia ni samaki wenye kuongiza lishe mwilini.

Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini, Mtumwa Peya Yussuf, aliitaka taasisi za uvuvi wa bahari kuja na utafiti utakao onesha mahitaji ya kilimo cha mwani na mazao mengine ya baharini.

Alisema mwani unakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na kupungua kwa uzalishaji na kwamba utafiti zaidi unahitajika kukabiliana na changamoto hizo.

"Tunahitaji kufanya utafiti ambao utatuwezesha kujua changamoto zinazokikabili kilimo cha mwani kupungua uzalishaji wake kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, walipitisha mswada huo ambao pamoja na mambo mengine utaweka masharti yanayohusu na kuendesha shughuli za uvuvi baharini katika maeneo ya hifadhi.




Masta Shangwe (katikati), akikabidhi mfano wa kadi ya bima kwa akinamama na watoto wao wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwananyamala, Dar es Salaam jana, itakayowawezesha kupata matibabu bure kwa kipindi cha mwaka mzima. Kupitia kampeni yake inayoendelea ya 'Sambaza Shangwe, Gusa Maisha', imekabidhi kadi za bima kwa akina mama na watoto wao jumla ya 600, ambapo kila hospitali itapokea 200 ikiwa ni zawadi ya upendo kutoka kwa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baraza la watu wenye ulemavu lakumbushwa usajili vikundi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amelitaka Baraza la watu wenye ulemavu kukamilisha usajili wa vikundi ili vifaidike na fedha za misaada inayotolewa na serikali.

Alisema idadi ya vikundi vya watu wenye ulemavu vilivyoomba mkopo ni 67 ambavyo havina usajili kwa ajili ya kupata mikopo hiyo.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikopo nafuu kwa kundi lenye mahitaji maalumu wakiwamo wenye ulemavu.

Alisema lengo la Serikali ya Zanzibar ni kuhakikisha makundi yote yenye mahitaji maalumu yanapata fedha za mikopo kwa ajili ya kufanya shughuli za kichumi na kujiletea maendeleo.

Aidha, alisema wizara ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ilipokea kutoka kwa Baraza la watu wenye ulemavu jumla ya vikundi 82 kwa ajili ya mikopo.

Alisema katika orodha hiyo vikundi vitano vimepatiwa mikopo yenye thamani ya jumla ya Sh. 31,000,000 wakati vikundi saba maombi yao yapo benki kwa ajili ya uchambuzi wa ziada.

"Vikundi 67 bado havina usajili kwa maana hiyo havina sifa ya kupata mikopo nalitaka baraza la watu wenye ulemavu kuvifuatilia na kupata usajili," alisema.

Soraga alisema kazi kubwa inayofanywa na wizara kwa kushirikiana na Shirikisho la Jumuiya ya watu wenye ulemavu (SHIWAZA) pamoja na baraza ni kutoa elimu zaidi ya umuhimu wa vikundi hivyo kukamilisha taratibu za usajili kwa ajili ya kupata mikopo.

Alisema wizara imetenga na kutoa kipaumbele kwa mikopo kwa watu wenye ulemavu kwa asilimia 20 ili wajikomboe na kujiwezesha kiuchumi na maendeleo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**FIXON ELIOT MTELESI** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 255041** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **3/12/2019.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/KIN/1462/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BLANCA MICHAEL TEMBA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0205/012** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIBOSHO GIRLS SEKONDARI** mwaka 1974. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **BUG/RB/5888/2012.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



NDG.SIMON I. MWAMBESO Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne (IV),chenye Index Na.S3187-0061,kilichotolewa na Baraza la mitihani Taifa kupitia shule ya sekondari Mtande mwaka 2019,iliyopo mkoa Mbeya-Chunya. Kwa yeyote atakayekiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
RIPOTI YA POLISI PHQ/MBE/CHU/6913/2023

## KUPOTELEWA NA CHETI



AIKAELI UNAMBWE MUNGURE anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1831/0001 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KILINGI SEKONDARI mwaka 2017. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/UBU/50550/2023.

## KUPOTEA KWA PASSPORT



NAJMA ABDI HASSAN naomba kutangaza kupotelewa kwa hati yangu ya kusafiria namba TAE325451 iliyotolewa uhamiaji makao makuu jijini DAR ES SALAAM. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/ILA/51358/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FRANCESCO PIERRE NINA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 662 APT – LANDCRUISER.** Chassis namba **UZJ1000076082.** Engine namba **2UZ0117932.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/8537/2023.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

AINEA YOSIA KATONDO anatangaza kupotea kwa hati ID No. 97120 ya kiwanja Plot 5, Block 24 kilichopo Chinangali East Jijini Dodoma. Yeyote atakayeiona atoe ripoti kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/32812/2023.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATE COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 25822 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GIDION LUKA MKUYE**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY:- ZAKARIA LUKAS MKUYE**

All persons claiming to have any interest in the estate of above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 20 day of 12/2023
DATED at MOROGORO this 04th day of DEC 2023

Resident Magistrate

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 95/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU PRIVA JOHN SWAI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA ESTA JOHN TESHA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa,
*Marehemu hakuacha wosia
*Futa isioyohusika
Imetolewa leo Tarehe 06 Mwezi 12 Mwaka 2023

............... ...........

**FOMU MADAI - 3**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASASI**
**Kituo cha LISEKESE Mkoa wa MTWARA**
**Shauri la Madai Na. 02/2023**
**KUITWA SHAURINI**
**(kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: ALI OMARY**
**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**KUPINGA MNADA ULIOFANYWA NA DALALI**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuri binafsi katika Mahakama hii tarehe 13 Mwezi wa 12 Mwaka 2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vilelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 05 Mwezi wa 12 Mwaka 2023.

Hakimu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya.........TANGA**
**Kituo cha MJINI TANGA........ MKOA.........TANGA**
**Usimamizi wa Mirathi Na......207/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ESTA MHINA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ANTHONY GUMBO DYAMWALE.**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo).**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika Shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 27 mwezi 12 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo Kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa Tarehe .....30...... mwezi...11.....2023

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**YA WILAYA MOROGORO MJINI**
**KITUO CHA KIHONDA**
**MKOA WA MOROGORO**
**SHAURI LA MADAI NA. 121/2023**
**JINA LA MDAI: JULLY MAARUFU MKWAYA**
**JINA LA MDAIWA: RAMADHANI NTEBE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu za madai katika Mahakama za mwanzo)**

**Kwa RAMADHANI NTEBE**

**Kwa kuwa mdai/Wadai ameleta/Wameleta Madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai):**

**Madai ya jembe la trecta na 1001 Box 1 yenye thamani ya Sh. 7800,000/=**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 14 Mwezi 12 Mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo vielelezo vyote vinavyo husu shauri hili kwaajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 24 mwezi 11 mwaka 2023.

HAKIMU

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0745 700 710.
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MIEZI MIWILI GAZA;

# UN: Gaza ni eneo hatari kwa mtoto

## • Milioni 1.9 wayahama makazi

Na Christina Mwakangale

WAKATI ikitimia miezi miwili ya vita huko Ukanda wa Gaza, zipo athari za kijamii zilizoripotiwa na vyombo vya habari vya kimataifa, ikiwamo vifo miongoni mwao wamo watoto na waandishi wa habari 81.

Umoja wa Mataifa (UN), umesema kwamba kwa sasa, eneo la Gaza ni miongoni mwa maeneo hatari zaidi kwa watoto duniani.

Kwa siku 60 huduma za kijamii maji, umeme zimekatizwa huku watoto 7,112 wakiuawa kati ya vifo vyote 16,248 vilivyotokana na vita hiyo tangu Oktoba 7, mwaka huu.

Kadhalika, wanawake 4,885 wamepoteza maisha huko Gaza kwa mujibu wa Al Jazeera, na kwamba wahudumu wa afya 284 wameuawa huku maofisa 132 wa UN, wakifariki dunia.

Umoja wa Mataifa (UN), umeitumia Ibara nadra huku Katibu Mkuu wa UN, Antonio Guterres, akituma ujumbe mzito kwa Baraza la Usalama kuhusu Gaza.

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), linasema huko Ukanda wa Gaza, hususan kusini mwa Gaza, kaya zinakumbwa na hali duni ya chakula.

WFP, inafafanua kwamba asilimia 97 ya kaya, kusini mwa Gaza, zina hali mbaya ya chakula huku kaya tisa kati ya 10 wakikosa mlo kwa siku nzima.

Kadhalika, linasema theluthi ya wakazi wa eneo la kusini, wanashuhudia kiwango kikubwa cha njaa huku asilimia 48 miongoni mwao hali ni mbaya zaidi.

WFP, linasema tangu Oktoba 7, mwaka huu, malori 1,249 yenye msaada wa chakula yalifika Gaza na kwamba awali kwa siku malori 500 yaliingia Gaza.

"Ili kutoa msaada wa chakula kwa walioathiriwa huko Gaza, kunahitajika malori 100 kila siku, lilisema shirika hilo

Shirika la Msalaba Mwekundu la Kipalestina (PRCS), huko Jabaliya, limesema linapokea takribani majeruhi 250 kwa saa linasema msaada wa asilimia 10 pekee ndio umewafikia waathiriwa.

### UMOJA WA MATAIFA

Akitumia ibara ya 99 kutoka katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ambayo ni nadra sana kutumia, Katibu Mkuu UN, Guterres ametoa wito kwa Baraza la Usalama kushinikiza kuepusha janga la kibinadamu.

Ametoa wito wa kuungana katika usitishaji kamili wa mapigano kati ya Israel na kundi la Kipalestina la Hamas.

Ibara hiyo ya 99 iliyoko katika Sura ya XV ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, inasema kwamba mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa "anaweza kulijulisha Baraza la Usalama jambo lolote ambalo kwa maoni yake, linaweza kutishia kudumisha amani na usalama wa kimataifa."

Katika taarifa kwa waandishi wa habari pamoja, Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Stephane Dujarric, alisema kuwa hii ni mara ya kwanza kwa Guterres, kuhisi kulazimishwa kutumia Ibara ya 99 tangu aingie madarakani mwaka wa 2017.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres. **PICHA: BBC**

Katika barua yake kwa Rais wa Baraza, Guterres alisema zaidi ya wiki nane za mapigano kwa ujumla zimesababisha mateso ya kutisha kwa binadamu, uharibifu wa kimwili na kiwewe cha pamoja kote Israel na eneo la Palestina, linalokaliwa kwa mabavu.

Ameangazia zaidi ya watu 1,200 waliouawa kikatili na kundi hilo, Oktoba 7, mwaka huu, ikiwa ni pamoja na watoto 33 na watu 130 wakiwa mateka.

"Lazima waachiliwe mara moja na bila masharti. Idadi za unyanyasaji wa kijinsia wakati wa mashambulio haya ni za kutisha," mkuu huyo wa Umoja wa Mataifa aliongeza.

Wakati Israel ikiendelea kuwalenga wapiganaji wa Hamas, Guterres alisema raia katika eneo lote la Ukanda huo, wanakabiliwa na hatari kubwa, huku zaidi ya watu 15,000 wakiripotiwa kuuawa, zaidi ya asilimia 40 wakiwa watoto.

Takriban asilimia 80 ya wananchi wa Gaza wameyakimbia makazi yao, zaidi ya watu milioni 1.1 wakitafuta hifadhi katika makazi ya Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi wa Palestina (UNRWA).

### KENYA YAONA FURSA ISRAEL

Kenya, imewapeleka wafanyakazi 1,500 wa mashambani nchini Israel, Wizara ya Kazi imesema.

Tangazo hilo linakuja takriban wiki mbili baada ya Malawi, kuwapeleka vijana 221 kufanya kazi katika mashamba ya Israel, na kusababisha lawama dhidi ya serikali.

Wafanyakazi hao wa kawaida watatumwa kwa kandarasi za miaka mitatu, inayoweza kuongezwa na mapato ya uhakika ya Dola za kimarekani 1,500 (£1,195).

Israel, imeigeukia Afrika, ili kuziba pengo kubwa la wafanyakazi kwenye mashamba yake, baada ya kuondoka kwa wingi kwa wafanyakazi wa kigeni.

Zaidi ya wafanyakazi 10,000 wa mashambani wahamiaji, wengi wao wakiwa raia wa Thailand, wameondoka Israel tangu kuanza kwa vita na Hamas mapema Oktoba, mwaka huu.

Israel, pia imewazuia kufanya kazi wafanyakazi wa Kipalestina, ambao walikuwa karibu asilimia 20 ya nguvu kazi ya kilimo kabla ya vita.

Wizara ya kilimo ya Israel, ililiambia CNN wiki iliyopita kwamba inahitaji wafanyakazi wa mashamba kati ya 30,000 hadi 40,000.

**UN/AL JAZEERA/BBC**

# Waziri wa Uhamiaji Uingereza ajiuzulu

**London, UINGEREZA**

ROBERT Jenrick, amejiuzulu kama Waziri wa Uhamiaji, akisema sheria ya dharura ya serikali ya Rwanda haijitoshelezi.

Alisema ulinzi madhubuti ulihitajika, ili kumaliza mfululizo wa changamoto za kisheria ambazo zinaweza kudhoofisha mpango huo.

Serikali ilisema muswada huo, uliozinduliwa mapema, uliweka wazi katika sheria za Uingereza, Rwanda, ilikuwa nchi salama kwa wanaotafuta hifadhi.

Lakini hauelezei kile ambacho baadhi ya wabunge wa Chama cha Kihafidhina cha Conservative wanachodai.

Katika barua yake ya kujiuzulu kwa Rishi Sunak, Jenrick alisema waziri mkuu ameelekea kwenye msimamo wake kuhusu sheria ya dharura.

"Hata hivyo, siwezi kuchukua sheria inayopendekezwa kwa sasa kupitia Bunge kwani siamini kwamba inatupa fursa nzuri zaidi ya kufaulu."

Jenrick aliongeza kuwa mswada huo ni ushindi wa matumaini dhidi ya uzoefu.

Serikali ya Rwanda imekuwa wazi kwamba haitakubali Uingereza kuegemeza mpango huu upande wa sheria ambayo inaweza kuchukuliwa kuwa inakiuka wajibu wetu wa sheria za kimataifa.

**BBC**



# SERIKALI YAIPONGEZA TSBA KUINUA MICHEZO TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKISHO la Kampuni za Ubashiri wa Michezo Tanzania (TSBA) limefanya mkutano mkuu wa tano wa mwaka ambapo imeweka azimio la kuendeleza shughuli za ubashiri wa michezo na kuunga mkono juhudi za maendeleo ya michezo nchini.

Pia mgeni rasmi katika mkutano huo, Halima Bulembo, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam aliipongeza TSBA kwa mchango wao mkubwa katika pato la taifa na kutambua mchango maalum wa shirikisho hilo katika kuwezesha timu za Tembo Warriors na Serengeti Girls kufanikisha ushiriki katika mashindano ya Kombe la Dunia mwaka jana.

Bulembo aliwahimiza waendeshaji wa kampuni za ubashiri wa michezo kuendelea kushiriki katika kuboresha miundombinu ya michezo na kusaidia mipango ya maendeleo ya michezo hapa nchini.

"Ninawasihi waendeshaji wa kampuni za ubashiri wa michezo kuendelea kuunga mkono mipango ya maendeleo ya michezo na kuboresha miundombinu ya michezo nchini," alisema.

Naye Mwenyekiti wa tatu na wa sasa wa TSBA, Sabrina Msuya, wakati akifungua mkutano huo kwa kutambua mchango wa watangulizi wake alitoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) na wanachama wote wa TSBA kwa ushirikiano wao thabiti kwa mwaka 2023 ambao ulikuwa na mafanikio makubwa. Msuya alieleza malengo muhimu ya shirikisho hilo kwa mwaka unaofuata, akisisitiza kuendeleza ushirikiano na taasisi za udhibiti, mpango wa mafunzo kwa wanachama wake, kutekeleza huduma za kijamii na juhudi za dhati za kulinda wateja.

Mkurugenzi wa Huduma wa GBT), Daniel Ole Sumayan, alipongeza juhudi kubwa zilizowaleta waendeshaji hao pamoja ili kuwa na sauti moja na ya uwakilishi katika tasnia ya ubashiri wa michezo.

Sumayan aliwahimiza wanachama wa TSBA kutumia jukwaa hilo kwa uwajibikaji na kwa maendeleo ya tasnia.

"Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania inaendelea kukuza mazingira mazuri ya udhibiti na kufanya kazi bega kwa bega na Shirikisho la Kampuni za Ubashiri wa Michezo Tanzania ili kupelekea mafanikio na ukuaji wa kiuwajibikaji wa tasnia hii nchini mwetu," aliongeza Sumayan.

TSBA lilianzishwa mwaka 2017 na limekuwa ni kiungo muhimu cha kuhamasisha juu ya ulinzi wa wachezaji, hasa kwa kampeni ya kupunguza kodi ya ushindi na kupambana na kampuni za ubashiri wa michezo zisizo na leseni nchini. Malengo haya makuu ya TSBA yanaendelea kuwa nguzo thabiti katika azma yao ya kuwa chombo cha uwajibikaji katika sekta ya ubashiri wa michezo.



Mchezaji wa Musoma Boys (kushoto), akijipanga kumtoka nyota wa Mshani Sports Academy katika mechi ya mashindano ya vijana wa umri chini ya miaka 17 iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza jana. Musoma Boys ilishinda mabao 3-1. **PICHA: TFF**

# Mwingira aibuka milionea mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Mkoa wa Ruvuma, Bernard Mwingira, ameibuka mshindi wa 'Jackpot' na kujinyakulia kitita cha Sh. milioni 250 kupitia Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya BetwayTanzania, imefahamika.

Akizungumza wakati wa kukabidhiwa hundi yenye kiasi hicho cha fedha katika hafla iliyofanyika jijini, Dar es Salaam jana, Mwingira alisema ushindi huo umempa faraja kubwa huku akiwataka wadau wengine wa mchezo huo kuendelea na kuamini kubashiri na kampuni hiyo.

"Sikutarajia kama ningeshinda kiasi hiki kikubwa cha fedha, nimekuwa nikishinda bashiri zangu nyingi ila siyo zenye kiasi kikubwa kama hiki cha fedha, ukweli najisikia furaha sana, nawasihi Watanzania wenzangu kuendelea kubashiri michezo mbalimbali ya kampuni hii ikiwamo Jackpot ili nao waweze kushinda," alisema Mwingira.

Mshindi huyo ambaye aliwasili Dar es Salaam juzi akitokea Ruvuma aliongeza kwake ushindi huo umekuja wakati mzuri hususani kipindi hiki ambacho ni msimu wa sikukuu na ameahidi kutumia fedha hizo kufanya mambo mbalimbali ya maendeleo ikiwamo kufungua biashara.

Pia mshindi huyo ameushukuru uongozi wa Betway Tanzania kwa ushirikiano waliomwonyesha na kusisitiza ataendelea kubashiri zaidi na zaidi kwa sababu kampuni hiyo inaaminika.

Naye Meneja Masoko wa Betway Tanzania, Calvin Mhina, mbali na kumpongeza mshindi huyo alisema kampuni yao imekuwa karibu na wateja wake wakati wote na kueleza malipo kwa mshindi hufanyika mapema na ni kielelezo cha uaminifu.

Aliongeza wao ndio kampuni bora ya ubashiri ulimwenguni na ushindi wa tuzo hiyo unawafanya kuendelea kujiweka mbele na kufanya promosheni nyingi nzuri zinazomwezesha mtu kushinda kwa urahisi.

## Kundemba, Malindi kibaruani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Kundemba FC inatarajia kukutana na Wekundu wa Mji Mkongwe, Malindi katika mechi ya raundi ya 14 ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mau B.

Timu zote zinashuka uwanjani zikiwa hazifanya vizuri katika mzunguko wa kwanza katika ligi hiyo yenye klabu 16 ambapo mwisho wa msimu zitateremka timu nne.

Kundemba ipo katika mstari wa hatari wa kushuka daraja ikiwa kwenye nafasi ya 13 baada ya kujikusanyia pointi 13 wakati wapinzani wao Malindi yenye pointi 15 iko kwenye nafasi ya 10.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Kundemba, Ali Vuai, alisema matarajio yake ni kuhakikisha timu yake inapambana na kushinda mchezo huo ili kujiondoa katika mstari wa hatari wa kushuka daraja.

Alisema anajua anaenda kukutana na timu ngumu na yenye uzoefu mkubwa katika Ligi Kuu Zanzibar lakini hilo halimzuii kuondoka na alama tatu katika mchezo huo na hatimaye kujiweka kwenye nafasi salama.

## Singida FG yapeleka Ligi Kuu Bara Karatu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya Uwanja wa CCM Liti uliopo mkoani, Singida kufungiwa, Singida Fountain Gate imetangaza kuhamia kwenye Uwanja wa Black Rhino Academy uliopo Karatu, jijini Arusha kwa ajili ya mechi zake za nyumbani za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Singida FG, Hussein Massanza, alisema timu hiyo itaanza kuutumia uwanja huo katika mechi dhidi ya KMC itakayochezwa Jumatatu.

Massanza alisema wameamua kuuchagua uwanja huo, baada ya mchakato na upembuzi yakinifu kufanyika na wanaamini hapo watakuwa salama katika michezo yao.

"Tulikuwa na mchaguo mengi kama vile Uwanja wa Jamhuri, Dodoma sehemu ambayo tunaijua vizuri sana, vile vile tulitaka kwenda Tabora kutumia Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi lakini kabla hatujafanya uamuzi tukasikia nao umefungiwa. Kikubwa tuliangalia uwanja wa jirani ambayo hata mashabiki wa Singida wanaweza kufika kwa urahisi," alisema Massanza.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMKOMALIA MBAPPE

REAL Madrid ipo tayari kumpa mshambuliaji wa Ufaransa na Paris St-Germain, Kylian Mbappe, mkataba mpya ifikapo Januari kabla ya kumalizika kwa mkataba wake wa sasa, lakini wababe hao wa Hispania watampa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 hadi Januari 15 kukubali au kukataa. **(AS)**

### RUCHARLISON ANUKIA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Richarlison analengwa na klabu za Ligi Kuu Saudi Arabia, lakini Tottenham Hotspur haina uwezo wa kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 isipokuwa inaweza kurejesha angalau pauni milioni 60 walizolipa kumsajili kutoka Everton. **(90 min)**

### GODFREY KUTUA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kumsajili beki wa Everton na Timu ya Taifa ya England, Ben Godfrey, mwenye umri wa miaka 25 katika dirisha la usajili la Januari. **(Sports)**

### CITY, UNITED VITANI

KLABU za Manchester City na Manchester United zote zinamtaka mlinzi wa Lille mwenye umri wa miaka 18, Mfaransa Leny Yoro, ambaye mkataba wake katika timu hiyo ya Ligue 1 utaendelea hadi Juni, mwaka 2025. **(Le10 Sport)**

### JUVE YAMTEMA SANCHO

KLABU ya Juventus iko tayari kujiondoa katika mpango wa kumsajili fowadi wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 23. **(Tuttosport)**

### MADUEKE KUONDOKA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Noni Madueke, mwenye umri wa miaka 21, ameonyesha nia ya kuondoka katika klabu hiyo ya London kwa vile hajafurahishwa na hatua ya kutochezeshwa. **(TeamTalk)**

### LAMPARD ANUKIA CHARLOTTE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard na kocha zamani wa Aston Villa, Dean Smith, watajwa kutakiwa katika timu ya Charlotte FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Soka Marekani. **(Mail)**

### LIVRAMENTO AITAKA ENGLAND

BEKI wa Newcastle United, Tino Livramento, mwenye umri wa miaka 21 ana haki ya kuichezea Timu za Taifa za Scotland na Ureno, lakini anataka kuthibitisha anatosha kuitumikia England. **(Telegraph)**

### LORENZO KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL inawania kumsajili fowadi wa Benfica na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Kyanno Lorenzo Silva, mwenye umri wa miaka 18. **(Football Insider)**

### CALHANOGLU KUIKAMUA WEST

IWAPO West Ham inataka kumsajili kiungo wa kati wa Inter Milan na Timu ya Taifa ya Uturuki, Hakan Calhanoglu, mwenye umri wa miaka 29 italazimika kulipa zaidi ya pauni milioni 40. **(Calciomercato)**

### COOPER AJIPANGA KUONDOKA

KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper, mwenye umri wa miaka 43, amewaambia marafiki zake amesikia mapendekezo ya kufutwa kazi na klabu hiyo. **(Football Insider)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATAKA USHINDI BILA RODRI

●●●Sasa City imepitwa pointi sita na vinara Arsenal ambao...

**LONDON, England**

PEP Guardiola amekiri Manchester City lazima itafute njia ya kushinda bila Rodri baada ya kushuhudia timu yake ikichapwa bao 1-0 na Aston Villa katika mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi usiku.

City walibakia na pointi zao 30 wakati vinara wa ligi hiyo, Arsenal wakiwa kileleni na pointi zao 36.

Bao lao la Leon Bailey katika kipindi cha pili liliipatia Aston Villa pointi tatu na kuwafanya City kucheza mechi nne za Ligi Kuu England bila ushindi msimu huu.

Nyota wa Hispania, Rodri alisimamishwa kwa safari hiyo na vipigo vitano vya mwisho vya City katika michuano yote vimetokea wakati ambapo amekosekana katika kikosi chao cha kwanza.

Baada ya mchezo huo, Guardiola alikubali timu yake lazima ijifunze kustahimili hali ya kutokuwepo kwa Rodri kwenye eneo la kiungo.

Alisema: "Rodri ni mchezaji muhimu bila shaka, lakini wakati hayupo lazima tutafute njia ya kushinda bila yeye.

"Tumepitwa pointi sita kileleni na tungekuwa kileleni mwa ligi lakini tulitoa sare tatu na kupoteza leo (juzi).

"Miaka iliyopita tumepata njia ya kushinda michezo, lakini tulijitahidi kidogo na lazima tutafute njia.

"Ni kazi yangu kupata suluhu. Mabadiliko ya nguvu kwa kushinda michezo. Wakati timu ni bora kuliko wewe, lazima utambue.

"Baada ya kuchezea mpira, tumefunga mabao manne au matano kwa pasi, hivyo ndivyo ilivyo na tunapaswa kukubali Aston Villa ilikuwa bora na sasa twende Luton."

City walikosa ubora wao wa kawaida na matokeo ya Villa yalikuja pale shuti la Bailey lilipomgusa Ruben Dias na kumpita golikipa, Ederson.

Ulikuwa ushindi uliostahili ambao ulifanya kikosi cha Unai Emery kusonga mbele juu ya mabingwa watetezi katika msimamo wa Ligi Kuu England hadi nafasi ya tatu.

City sasa itasafiri hadi Luton Jumapili na Rodri atakuwepo.

# TEN HAG: UNITED HATUNA MIGOGORO



**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag alisema Manchester United haijawa klabu ya mgogoro msimu huu licha ya vichwa vya habari vibaya na msururu wa matokeo mabaya baada ya mabao mawili ya Scott McTominay kuipatia ushindi wa magoli 2-1 Old dhidi ya Chelsea juzi kwenye Uwanja wa Trafford.

United ilipata ushindi huo licha ya Marcus Rashford kuwekwa benchi umeifanya timu hiyo ya Ten Hag kupunguza tofauti ya pointi hadi tatu dhidi ya mabingwa watetezi Manchester City, ambao wako katika nafasi ya nne baada ya kufungwa 1-0 na Aston Villa.

Lakini huku Ten Hag akiwaacha Rashford na Anthony Martial kufuatia matokeo duni katika mechi ya Jumamosi waliyochapwa 1-0 na Newcastle United, kocha huyo alikataa mapendekezo klabu yake imekuwa katika mgogoro wiki za hivi karibuni.

"Mgogoro? Sio kwa ajili yetu," alisema Ten Hag. "Tupo safarini, tumetulia na kuamini mchakato ulivyo, tunajua tunachopaswa kujenga na hatubabaiki na ukosoaji unaotuzunguka, sijali kelele, tunaposhikana tuwe na mtazamo sahihi, tuna maonyesho ya kukusanya pointi.

"Unaona jinsi tulivyoshinda pointi, tulitawala dhidi ya mpinzani wetu kwa kumiliki mpira na hivyo ndivyo tunavyotaka kucheza."

United walikuwa na mashuti 28, tisa yaliyolenga lango huku walipokuwa wakitawala timu hiyo ya Mauricio Pochettino pale Old Trafford.

Na ingawa bao la Cole Palmer la dakika ya 44 lilisawazisha lile la kwanza la McTominay, kiungo huyo wa United alirejesha uongozi wa timu ya nyumbani na kuipa ushindi kwa bao la kichwa kipindi cha pili.

"Mwishoni tulishinda, lakini tungeweza kurahisisha maisha," alisema Ten Hag. "Tungeweza kufunga mara tatu katika dakika 30 za kwanza.

"Tunajua hatujaridhika haraka na kuwa na furaha kwa sababu tunataka kufanya vizuri zaidi na kuweka mambo sawa. Lakini nimefurahishwa sana na idadi ya nafasi tulizotengeneza."

United watawakaribisha Bournemouth kwenye Uwanja wa Old Trafford katika mechi ijayo ya Ligi Kuu England.

# Santos yashushwa daraja Brazil

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

MOJAWAPO ya misimu ya kusisimua ya Ligi Kuu Brazil iliyomalizika juzi kwa timu imara zaidi ya msimu huu, Palmeiras kutetea taji lake na klabu ambayo ilikuwa nyumbani kwa marehemu Pele, Santos ikishuka daraja kwa mara ya kwanza.

Palmeiras ilitoka sare ya 1-1 na Cruzeiro na kutawazwa mabingwa wa Brazil kwa mara ya 12. Endrick mwenye umri wa miaka 18 alifunga bao lake la 11 msimu huu na kuipa Palmeiras goli la mapema na Nikao kusawazisha dakika ya 80 mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mineirao kule Belo Horizonte.

Kushushwa daraja kwa Santos kufuatia kufungwa 2-1 nyumbani na Fortaleza ilikuwa kikwazo kingine kwa klabu hiyo kwenye uwanja ambapo mazishi ya Pele yalifanyika Januari, mwaka huu.

Timu hiyo kutoka jiji la Pwani, ilikuwa moja ya klabu tatu pamoja na Sao Paulo na Flamengo, ambazo hazijawahi kushushwa daraja kutoka kwenye Ligi Kuu Brazil lakini mwendo mbaya wa michezo mitano bila ushindi uliwafanya kushuka hadi nafasi ya 17 katika msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 43.

Ubingwa wa mwaka huu ulikwenda kwa Palmeiras huku mshambuliaji, Endrick, ambaye anatarajiwa kujiunga na Real Madrid, akifunga mabao kadhaa muhimu na mpinzani wake Botafogo akipoteza uongozi wa pointi 13.

Atlético Mineiro na Flamengo, ambazo zilikuwa na nafasi ndogo ya kushinda kombe katika raundi ya mwisho, zilipoteza mechi zao. Vipigo hivyo viliiruhusu Gremio ya Luis Suárez kumaliza katika nafasi ya pili baada wa ushindi wa 3-2 dhidi ya Fluminense, huku mshambuliaji huyo wa Uruguay akifunga mabao mawili. Nyota wa zamani wa Brazil, Pele aliisaidia Santos kuwa moja ya klabu maarufu katika soka la dunia, timu hiyo ikifurahia enzi za dhahabu katika miaka ya 1950 na 1960 ambayo iliwafanya kushinda mataji 10 ya majimbo na sita ya ligi ya Brazil.

# Klopp alalamikia ratiba ngumu EPL

**SHEFFIELD, England**

JURGEN Klopp aliibua hasira nyingine kuhusu upangaji ratiba wa Liverpool baada ya kuona timu yake ikishinda Sheffield United 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu England (EPL) uliochezwa juzi usiku.

Baada ya mabao kutoka kwa Virgil van Dijk na Dominik Szoboszlai kufikisha pointi 34 ikipitwa mbili na vinara Arsebal kwenye uwanja wa Bramall Lane, wekundu hao sasa watakabiliwa na mchezo mwingine chini ya saa 72 watakapoelekea Crystal Palace Jumamosi.

Kocha huyo wa Ujerumani amekuwa na tabia ya kuonesha hasira zake kutokana na orodha nyingi za mechi katika miaka iliyopita na hakumkubali mhojiwa baada ya mechi kwa kejeli akimwambia kwamba "wakati anaopenda zaidi wa kuanza" ndio unaofuata kwenye ajenda.

Klopp alijibu: "Huo ni ujasiri sana kwako kufanya mzaha kuhusu hilo.

Liverpool hawakuwa katika ubora wao, lakini walikuwa na nafasi nzuri za kufunga katika mchezo huo.

Van Dijk alipachika wavuni bao kutokana na kona ya Trent Alexander-Arnold dakika ya 37 na kuwanyamazisha mashabiki wa nyumbani, ambao walikuwa wameona timu yao inayokabiliwa na matatizo ikianza vyema.

Nahodha huyo wa Liverpool alikiri kufarijika kwake kuona mpira ukigonga wavu kwa bao lake la kwanza la msimu huu.

Van Dijk alisema: "Unapopata nafasi ya bure kama hiyo lazima umalize. Ninafurahi kwamba nilifanya.

"Ni bao muhimu hasa unapojaribu kupiga shuti la chini."

"Ni wazi lazima ufanye kazi kwa kila mchezo, haswa dhidi ya timu ambayo ilibadilisha kocha. Ilikuwa unaenda vitani, lakini tulifanya vizuri na tulistahili alama tatu."

Katika sekunde chache za mwisho za mchezo, Darwin Nunez alishinda mpira kutoka kwa Jayden Bogle na kumwanzishia mchezaji wa kimataifa wa Hungary, Szoboszlai, ambaye alifunga kwa urahisi.

Ushindi huo unamaanisha kwamba Liverpool sasa wamepitwa pointi mbili tu wakiwa nafasi ya pili dhidi ya vinara Arsenal.

# BENCHIKHA ATEMA CHECHE, APATA DAWA 'KUIUA' WYDAD

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikitamba tayari imepata dawa ya kuizuia Wydad Casablanca katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa nyumbani kwao, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha, amesema hataki wachezaji wavivu na wasiojituma katika kikosi chake.

Akizungumza kutoka mjini Marrakech jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema walipata muda wa mzuri wa kuwashuhudia wapinzani wao wakicheza mechi ya Ligi Kuu Morocco dhidi ya MC Oudja na kushinda mabao 3-1 ambapo benchi la ufundi limepata muda wa kuwasoma Waarabu hao.

Matola alisema kupitia mechi hiyo wameifuatilia kwa karibu Wydad na tayari baadhi ya vitu wameshaanza kuvifanyia kazi.

"Haya ni masuala ya kiufundi sitazungumza sana, lakini hata kama hawatacheza kama walivyocheza katika mechi hiyo, lakini kuna asilimia nyingi hawatabadilika sana," alisema Matola.

Kuhusu mchezo wa raundi ya tatu ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Marrakech, Matola alisema utakuwa mgumu kwa pande zote mbili, lakini kwao wamejipanga kuhakikisha wanatimiza lengo lao la kutopoteza pointi.

"Siyo kama Wydad Casablanca ilipoteza mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa makusudi, hapana, ilitaka kushinda lakini ilipoteza kwa sababu uwezo au ilizidiwa mbinu na timu ilizokutana nazo, kwa hiyo hata mechi yetu sisi hawatakuja eti wafungwe tu kirahisi, kwa sababu hii kwao ni kama mechi ya fainali inabidi ipate ushindi ili irejee kwenye njia sahihi ya kwenda robo fainali.

Sisi Simba pia tunalitambua hilo na tunajua haitakuwa mechi rahisi, ni ngumu sana, lakini tutaingia uwanjani kupambana na kuondoka na pointi, tutacheza kwa umakini na utulivu," alisema Matola.

Hata hivyo alisema Simba pia ni klabu kubwa na yenye malengo makubwa, hivyo na watacheza mechi hiyo kwa kuwabana wenyeji ili kushinda au kuvuna pointi moja muhimu na kuweka hai matumaini ya kusonga mbele.

"Pointi ambazo Wydad Casablanca inazihitaji na sisi tunazihitaji, na sisi pia ni kama fainali, ili tuwe katika njia sahihi ya kusonga mbele ni lazima tupate matokeo ambayo si ya kufungwa, tushinde au kutoka sare na hilo ndilo tunalipogania," Matola aliongeza.

Alisema mabadiliko ya uchezaji katika kikosi chao ni kitu ambacho kinampa matumaini.




Mchezaji mkongwe wa tenisi duniani, Patrick McEnroe, akijiandaa kupiga mpira katika mashindano ya McEnroe Serengeti Cup yaliyofanyika juzi kwenye Mbuga ya Serengeti iliyoko kwenye mkoa wa Mara na Arusha na kudhaminiwa na Benki ya KCB. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mashujaa, Prisons hapatoshi Kigoma

**Na Saada Akida**

IKIWA katika hali tete, Mashujaa FC inatarajia kuwakaribisha Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani, Kigoma huku Ihefu SC ikiwaalika Tabora Uited kwenye dimba la Highlands Estates ulioko Mbarali, Mbeya.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa Tanzania Prisons, Ajabu Kifukwe, alisema timu yake imejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na wamejipanga kurekebisha makosa yaliyojitokeza kwenye mechi zilizopita.

Kifukwe alisema baada ya mechi ya leo kumalizika, wanatarajia kupokea ripoti kutoka katika benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha, Ahmad Ally, ili kuanza mikakati ya mchakato wa usajili wa wachezaji wapya.

Alisema wanahitaji kuimarisha kikosi chao kwa kufanya maboresho kwa kuzingatia mapendekezo yatakayotolewa na benchi la ufundi ili kuingia katika mzunguko wa pili wakiwa imara.

"Kesho (leo) tuna mchezo dhidi ya Mashujaa FC, baada ya mechi hiyo tutapokea ripoti kutoka kwa kocha Ahmad, itatueleza nafasi anazotaka kuboresha lakini pia ni mchezaji gani anamhitaji ili kuongeza nguvu kwa kuzingatia mapungufu aliyoyaona," alisema Kifukwe.

Aliongeza anaamini wachezaji watakaowasajili watakiongezea nguvu kikosi kwa kushirikiana na nyota watakaowakuta ili kufikia malengo na kuacha kucheza kwa presha ya kujinasua na janga la kushuka daraja.

Kiongozi huyo alisema watakuwa makini katika mchakato huo wa usajili kwa sababu wanahitaji kuongeza nguvu ili kufikia malengo ya kufanya vizuri kwenye michezo iliyopo mbele yao ya Ligi Kuu na michuano ya Kombe la FA.

# Yanga yasaka pointi muhimu CAF

INATOKA UK. 24

tutakuwa na morali kubwa," Mwamnyeto alisema.

Kibabage alisema mechi ya leo ni muhimu na wanawaahidi wanachama wao watapambana ili kupata kile walichokifuata.

"Ukiingalia Medeama ni timu kubwa, ni klabu kubwa, tunawaahidi Wana-Yanga tutafanya vizuri, tunaomba Watanzania watuombee dua ili tupate pointi tatu, turejee nyumbani tukiwa na furaha," Kibabage alisema.

Msimu uliopita Yanga ilicheza fainali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho dhidi ya mabingwa, USM Alger ya Algeria.

# Rais Samia awapa Twiga Stars 200m/-

INATOKA UK. 24

Athumani Nyamlani, alimshukuru Rais Samia kwa motisha aliyotoa kwa wachezaji wa Twiga Stars ili waendelee kuipambania nchini katika mashindano yaliyopo mbele yao.

"Tunawashukuru Watanzania kwa sala zao, serikali kwa kutuwezesha kufika hapa, kwa kutusaidia tiketi za safari na mambo mengine, katika mashindano lazima kuwe na maandalizi mazuri ambayo tulifanya awali na imetusaidia kufikia hapa.

Mechi yetu ilikuwa ya ushindani mkubwa lakini wachezaji walipambana kupigania taifa lao na hatimaye tumefanikiwa kucheza fainali, tunaendelea kuweka mkazo katika maandalizi kwa sababu sasa katika soka la wanawake Tanzania ni nchi kubwa na tishio," alisema Nyamlani.



Michezo

Ijumaa Desemba 8, 2023

Nipashe



## Guardiola ataka ushindi bila Rodri

UKURASA 21



# YANGA YASAKA POINTI MUHIMU CAF

## Yawakabili Medeama ugenini Ghana, Gamondi atamba...

Kiungo wa kimataifa wa Yanga kutoka Uganda, Khalid Aucho akifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya Kundi D ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Medeama SC itakayochezwa leo mjini Kumasi, Ghana. **PICHA: MTANDAO**

**Na Saada Akida**

ILI kujiweka katika mazingira bora ya kusonga mbele kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga ikiwa ugenini kuwavaa Medeama, inahitaji matokeo ya ushindi kwa ajili ya kufufua matumaini ya kusonga mbele katika michuano hiyo.

Mechi hiyo ya tatu katika ya Kundi D itachezwa kwenye Uwanja wa Baba Yara uliopo Kumasi, Ghana kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Yanga ambayo ilianza hatua hiyo ya makundi kwa kupokea kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa CR Belouizdad ya Algeria na sare ya nyumbani ya bao 1-1 dhidi ya Al Ahly ya Misri, inaburuza mkia katika kundi hilo na ili kurejesha matumaini ya kusonga mbele inahitaji matokeo ya ushindi tu.

Endapo Yanga itashinda katika mechi ya leo, itafikisha pointi nne na kuondoka mkiani huku ikiwaombea dua mbaya vinara wa kundi hilo Al Ahly yenye pointi nne itakayowakaribisha nyumbani CR Belouizdad.

Matokeo ya sare yoyote hayatakuwa na afya kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sababu watafikisha pointi mbili na kusalia mkiani katika kundi hilo wakati wakiwa na kumbukumbu ya kutocheza hatua ya makundi kwa miaka 25.

Kama Yanga itapoteza mechi ya leo, itatakiwa kuhakikisha inashinda mechi zake tatu zilizosalia, mbili dhidi ya Medeama na CR Belouizdad wakicheza nyumbani na moja watakapowafuata Al Alhy nyumbani kwao Cairo.

Kuelekea mchezo wa leo, Yanga itakosa huduma ya beki wake, Joyce Lomalisa, ambaye anauguza jeraha la mguu na nafasi yake huenda ikachukuliwa na Nickson Kibabage.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema kikosi chake kipo tayari kwa mechi hiyo na anafahamu ugumu wa kukabiliana na wapinzani wao.

Gamondi alisema Yanga imejipanga vizuri kusaka ushindi na anaamini hakuna mechi rahisi katika mashindano hayo na hasa timu yako inapocheza ugenini.

"Tunawaheshimu wapinzani wetu, ni timu nzuri inayoundwa na wachezaji bora na wamekuwa na wastani mzuri wa kupata bao kila mechi. Hatuna nafasi ya kusema tunajilinda, kitu muhimu ni kucheza kwa nidhamu kubwa ya kulinda na kutafuta ushindi," alisema Gamondi.

Aliongeza kila mchezaji anatambua umuhimu wa mchezo huo wanatarajia kutumia vizuri nafasi watakazotengeneza ili kufikia kufufua matumaini ya kufikia malengo ya kucheza hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, alisema wamejipanga vyema kuondoka na ushindi na wanaamini wakipata pointi tatu, watarejesha morari kwenye kikosi chao ambacho kilianza vibaya hatua hiyo.

"Walioko huku wote ni mabingwa, tunajua umuhimu wa mechi hii, katika mashindano haya hakuna timu ndogo, tunachotaka ni kuingia uwanjani kupambana, tutakaposhinda mechi ya kesho (leo), kundi litakuwa wazi kwa kila timu,

INAENDELEA UK. 23

# Rais Samia awapa Twiga Stars 200m/-

**Na Saada Akida**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, ametoa Sh. milioni 200 kwa kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars ) kama zawadi ya kufanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (WAFCON 2024), zitakazofanyika Morocco, mapema mwakani.

Twiga Stars iliyorejea nchini jana alfajiri ikitokea Togo, ilipata tiketi ya kucheza fainali hizo kwa ushindi wa jumla wa mabao 3-2, ikishinda magoli 3-0 nyumbani na kuchapwa mabao 2-0 ugenini.

Akizungumza jijini, Da es Salaam jana Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, alisema Rais Samia anawapongeza Twiga Stars kwa mafanikio waliyopata na ametoa fedha hizo kwa ajili ya kuwapongeza ari wachezaji hao walioipeperusha vyema bendera ya Tanzania.

Ndumbaro alisema ni jambo la kujivunia kwa sababu Tanzania ndio nchi pekee iliyofanikiwa kukata tiketi ya kucheza fainali za WAFCON na AFCON kutoka kwenye Ukanda wa nchi 13 wanachama wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

"Niwapongeze wachezaji na benchi la ufundi kwa kupigania taifa, nina salamu kutoka kwa Rais wetu ametoa kiasi cha milioni 200 ikiwa ni bonasi kwa hatua iliyofikia timu yetu. Ushindi huu unaongea mambo mengi sana.

Soka la Tanzania upande wa wanawake limekuwa na limepiga hatua nzuri, lakini maendeleo hayo hayaendi bila ya uchumi ambao nao umekuwa," alisema Ndumbaro.

Aliongeza watatumia fursa hiyo kuhakikisha watu na wafanyabiashara kujitokeza katika kuwekeza katika soka la wanawake pamoja na michezo mingine ili kupiga hatua kubwa zaidi.

Makamu wa Kwanza wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF),

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >